

**UPIMAJI WA UFAHAMU WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA
KUFUNDISHIA SHULE ZA MSINGI: MIFANO KUTOKA HALMASHAURI
YA WILAYA YA GEITA**

JUMA MOHAMED KUTEYA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA
LUGHA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2019

UTHIBITISHO

Aliyeidhinisha hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa ;
"Upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi : mifano kifani toka halmashauri ya wilaya ya Geita", na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya utahini wa shahada ya uzamili (MA - KISWAHILI) katika isimu ya kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....
Dkt. Zelda Elisifa

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKI MILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kuigwa, kukaririwa, kunakiliwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote iwayo au kuhawilishwa kwa mbinu yoyote ile; ya kielektroniki, kunakili, kurudufu katika hali yoyote bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi, **Juma Mohamed Kuteya**, natamka na ninathibitisha kwamba tasnifu hii inayoitwa: Upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi: mifano kifani toka halmashauri ya wilaya ya Geita, ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba hajjawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

.....
Juma Mohamed Kuteya

.....
Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii namtabaruki (marehemu) mama yangu mzazi Bi Hawa Hamisi Nyunda. Pia namtabaruki (marehemu) baba yangu mzazi Mzee Mohamed Kuteya Mkanga, wazazi wangu hawa walinilea kwa wema na kunifanya niwe na kiu ya masomo ili niweze kufaulu maishani na walitoa michango yao mbalimbali ya hali na mali kuwezesha masomo yangu nilipokuwa bado ni tegemezi. Daima nitakumbuka yote mliyofanya kwa ajili ya maisha yangu. Namuomba Allah mtukufu awalipe Jannatul Firdaus ‘Aamin’

SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu aliyenijaalia uhai, nguvu, fikra na uwezo wa kuandika na kukamilisha kazi hii. Kwa hakika bila msaada wake lolote haliwezi kufanyika. Tasnifu hii imekamilika kutokana na msaada mkubwa wa Allah Subhana Wataala. Ninasema Alhamdu lillah Rabil ghaalamiin.

Pili Shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu wa utafiti huu mpendwa, Dk. Zelda Elisifa wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa kubeba jukumu la kusimamia vyema kazi hii. Ninamshukuru kwa Uzoefu wake binafsi, uvumilivu, ujasiri, upendo, hekma na ushauri wake mkubwa tokea hatua za mwanzo za kuandika pendekezo la utafiti hadi kumalizika kwa kazi hii. Ninaamini kuwa amenivumilia vya kutosha kwa udhaifu wangu kama binaadamu na kama mwanafunzi. Mafanikio ya tasnifu hii yametokana na juhudi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha, kuelekeza na kushauri yale yote yanayofaa kuzingatiwa katika utafiti huu. Licha ya majukumu mengi aliyonayo, hakisita hata mara moja kusoma kazi yangu kwa umakini mkubwa, kwa wakati na kutoa maelekezo yanayojenga kazi yangu kwa umakini mkubwa. Sina cha kumlipa ila namuombea kwa Allah ampe maisha marefu na mema ili aweze kuendelea kutoa mchango wake kwa wanataaluma wa taifa kwa ujumla.

Tatu, kwa moyo mweupe napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania idara ya Isimu na Taaluma za Fasihi kwa kuweza kuanzisha shahada ya uzamili ya Kiswahili na kunichagua mimi kuwa ni mmoja wao kati ya wanafunzi wa Isimu waliochaguliwa kujiunga katika Chuo hiki pamoja na

wahadhiri wote waliotumia muda wao kunifundisha wakati wa mihadhara ya darasani na maelekezo mbambali ya msingi wakiongozwa na: Dk. Nestory Ligembe, Dk. Hanna Simpassa, Dkt. Hadija Jilala, Dkt Dunlop Ochieng, Dkt Mohamed Omary Maguo na Dk. Pembe Lipembe wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa jinsi walivyojitoa wakati wote kunifundisha, kuendeleza na kukamilisha maarifa na stadi zilizohitajiwa ili kukamilisha kiwango cha shahada hii. Mungu awape maisha marefu na ya furaha katika maisha yao yote ili waendeele kutoa mchango wa kitaaluma na wa kijamii katika taifa letu, na yule atayetangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu ampe haki yake anayostahiki.

Halikadhalika, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya uzamili ya Kiswahili wa mwaka wa masomo 2017/2018. Shukurani hizi za pekee zimetokana na ushirikiano wao wa dhati walionipatia katika maswala ya taaluma kwa kipindi chote cha masomo ya uzamili. Mungu awazidishie moyo wa kusaidiana na kupendana katika taaluma. Vilevile, ninatoa shukurani zangu za aina yake kwa familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa Mwanvita Shabani, watoto wangu wapendwa, Shamila, Shadya, Shakila, Shafii na Sharifa kwa upendo na uvumilivu wao wakati wote nilipokuwa nasoma, upo wakati walinihitaji lakini kutokana na majukumu ya usomaji na kazi hii muhimu haikuwezekana nawashukuru tena kwa uvumilivu wao

Aidha shurani za kipee ziwaendee wafanyakazi wenzangu wa idara ya Uthibiti ubora wa shule wilaya ya Geita (v) wakiongozwa na Mthibit ubora mkuu Bwana Dismas

Manyonyi, Bwana Wilson Kashaga na bwana Elikana Luchagula bila kumsahau Jene Mlawwa kwa uvumilivu na ushikiano walionipa wakati wa kipindi chote cha masomo. Mwisho nawashukuru kwa ujumla, watu wote waliotoa michango yao hadi kumalizika kwa kazi hii ni wengi sana na vigumu kuwataja wote katika wasaa huu. Ila nawaomba waamini kuwa michango yao imepokelewa kwa moyo mkunjufu na imesaidia kufanikisha kazi hii na Mungu awajaze imani na baraka katika maisha yao na awape moyo huo huo wa kusaidiana katika shughuli nyengine ziwe za kitaaluma au nyenginezo.

IKISIRI

Utafiti ulilenga kufanya upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi kwa wanafunzi wa darasa la VII katika halmashauri ya Geita. Utafiti ulifanyika ili kutoa mchango wa kitaaluma katika lugha ya kufundishia shule za msingi kuona ufahamu walio nao wanafunzi. Lengo la utafiti ni kupima ufahamu wa wanafunzi katika lugha kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi na Malengo Mahususi yalikuwa ni kupima ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa shule za msingi Geita na Kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia shule za msingi. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981), ili kuweza kutimiza malengo ya utafiti huu na pia kujibu maswali ya utafiti huu. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia njia ya zoezi la umilisi wa lugha, usaili, hojaji na mbinu ya usomaji wa nyaraka. Eneo la utafiti lilikuwa wilaya ya Geita, kata ya Nyakamwaga. Walengwa wa utafiti huu walikuwa ni wanafunzi wote wa darasa la saba na sampuli ya utafiti ilikuwa ni wanafunzi 20 toka shule hizo 5 ambapo jumla yake ni watafitiwa 100. Watafitiwa hao waliosailiwa na kujibu maswali ya hojaji na pia maswali ya zoezi la umilisi wa lugha. Watafitiwa waliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha unasibu. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kitakwimu. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa wanafunzi wana ujuzi na ubobezi katika lugha ya kufundishia hivyo wana ufahamu wa kutosha katika vipengele ambavyo mtafiti aliwapima katika lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi. Ufahamu wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili unakidhi vigezo vyote vya kutumia lugha hiyo katika kufundishia na kujifunzia shule za msingi.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	i
HAKI MILIKI	ii
TAMKO	iii
TABARUKU	iv
SHUKRANI	v
IKISIRI	viii
YALIYOMO	ix
ORODHA YA MAJENDWALI	xiii
ORODHA YA MICHORO.....	xiv
ORODHA YA UFUPISHO	xv
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Mada	1
1.2 Tatizo la Utafiti	11
1.3 Malengo ya Utafiti	12
1.3.2 Malengo Mahususi	12
1.4 Maswali ya Utafiti.....	13
1.5 Umuhimu wa Utafiti	13
1.6 Mipaka ya Utafiti	14
1.7 Hitimisho	14
SURA YA PILI	15
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI	15
2.1 Utangulizi	15

2.2	Dhana ya Lugha, Uamiliaji Lugha na Ujifunzaji Lugha	15
2.3	Lugha ya Kufundishia	17
2.4	Lugha Rasmi za Kufundishia na Kujifunzia Tanzania.....	20
2.5	Dhana ya Upimaji	23
2.6	Mapitio ya kazi Tangulizi.....	25
2.7	Kiunzi cha Nadharia.....	30
2.7.1	Nadharia ya Umilisi Wa Mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981).....	32
2.8	Pengo la Utafiti	33
2.9	Hitimisho	34
	SURA YA TATU	35
	MBINU ZA UTAFITI.....	35
3.1	Utangulizi	35
3.2	Usanifu na Mkabala wa Utafiti.....	35
3.3	Eneo la Utafiti.....	36
3.4	Sampuli na Usampulishaji.....	37
3.4.1	Sampuli.....	37
3.4.2	Usampulishaji	37
3.5	Vyanzo vya Data.....	38
3.5.1	Data za Msingi	38
3.5.2	Data Upili	38
3.6	Mbinu za Kukusanya Data	39
3.6.1	Zoezi la Umilisi.....	39
3.6.2	Mbinu ya Hojaji	39

3.6.3	Mbinu ya Mahojiano /Usaili.....	39
3.6.4	Mbinu ya usomaji wa nyaraka.....	41
3.7	Maadili ya Utafiti.....	41
3.8	Uchambuzi wa Data.....	42
3.9	Muhutajari.....	42
	SURA YA NNE.....	43
	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....	43
4.1	Utangulizi.....	43
4.2	Ubobezi wa Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi.....	44
4.2.1	Tathmini binafsi ya Ujuzi au Ufahamu Katika Lugha ya Kiswahili.....	45
4.2.2	Ufahamu wa Wanafunzi katika Kutambua na Kubaini Aina za Maneno	45
4.2.3	Uwezo wa Wanafunzi katika Matumizi ya Msamiati na Usanifu wa Lugha.....	51
4.2.4	Ufahamu katika Muundo wa Sentensi	53
4.2.5	Utambuzi wa Matumizi ya Nafsi katika Tungo.....	55
4.2.6	Ufahamu wa Matumizi ya Njeo.....	57
4.2.6.1	Ufahamu wa Matumizi ya Njeo Katika Sentensi.....	57
4.2.6.2	Uwezo Wa Wanafunzi Kutunga Sentensi Kwa Kutumia Mofimu za Njeo	58
4.2.7	Uelewa wa Watafitiwa katika Utumizi wa Lugha	61
4.2.8	Sababu Zinazochangia Watafitiwa Kuwa Na Ufahamu Katika Lugha ya Kiswahili.....	63
4.3	Kutathmini Kiwango cha Ubobezi wa Kiswahili Dhidi ya Sifa za Lugha ya	

Kufundishia Shule za Msingi.....	71
4.3.1 Ubobezi Uliopimwa Dhidi ya Sifa za Lugha ya Kufundishia	66
4.3.2 Ushahidi wa Ubobezi wa Kiswahili katika mitihani ya ndani.....	70
4.4 Hitimisho	83
SURA YA TANO	78
MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	78
5.1 Utangulizi	78
5.2 Muhutasari wa Utafiti.....	78
5.2.1 Muhutasari wa Jumla	78
5.2.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti	79
5.3 Hitimisho	80
5.4 Mapendekezo	81
5.4.1 Mapendekezo ya Jumla	81
5.4.2 Mapendekeo kwa Tafari Zijazo	81
MAREJEO	82
VIAMBATANISHO	90

ORODHA YA MAJENDWALI

Jedwali 4.1 : Idadi ya Wanafunzi Wa Darasa la Saba Katika Shule za Kata ya Nyakamwaga	47
Jedwali 4.2: Matokeo ya Watafitiwa Kuhusu Ufahamu au Ujuzi wa Lugha ya Kiswahili.....	48
Jedwali 4.3 : Matokeo Kubaini na Kutambua Aina aa Maneno.....	51
Jedwali 4.4: Matokeo ya Matumizi ya Msamiati Sahihi na Usanifu wa Lugha.....	54
Jedwali 4.5 : Ufahamu wa Matumizi ya Muundo wa Sentensi Katika Upatanisho Wa Kisarufi.....	56
Jedwali 4.6 : Matokeo Kuhusu Kutambua Matumizi ya Nafsi katika Tungo	59
Jedwali 4.7: Ufahamu wa Matumizi ya Njeo	61
Jedwali 4.8: Ufahamu wa Matumizi ya Njeo	63
Jedwali 4.9 : Matokeo ya Watafitiwa Kuhusu Uelewa wa Watafitiwa Katika Utumizi Wa Lugha	65
Jedwali 4.10: Watafitiwa Waliokuwepo Wakati wa Usaili	69
Jedwali 4.11: Matokeo ta Ufaulu wa Wanafunzi Kwa Somo la Kiswahili.....	77
Jedwali 4.12 : Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi Kwa Somo la Maarifa ya Jamii.	78
Jedwali 4.13: Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi kwa Somo la Hisabati.....	79
Jedwali 4.14: Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi Kwa Somo ya Sayansi	80
Jedwali 4.15 : Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi kwa Somo la Kiingereza.....	81

ORODHA YA MICHORO

Mchoro 4.1 : Maswali na Majibu kwa ajili ya Wanafunzi.....	50
Mchoro 4.2 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali 1-3	53
Mchoro 4.3: Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Nne	55
Mchoro 4.4 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Saba	58
Mchoro 4.5: Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa	60
Mchoro 4.6: Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Tisa	62
Mchoro 4.7 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Nne	64
Mchoro 4 :8 ushahidi juu lugha wanayotumia wanafunzi.	67
Mchoro 4.9 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la 4.....	68

ORODHA YA UFUPISHO

BAKITA	Baraza la kiswahili Tanzania
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
SAMIKISA	Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu
LOITASA	Languages of instruction in Tanzania and South Africa.
UNESCO	United Nations Educational, Scientific, and Cultural Organization

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu umejikita katika upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi. Lugha ya kufundishia ni lugha maalumu inayoteuliwa kutumika kutolea elimu rasmi katika taifa husika. Sera ya elimu (2011:38) inaeleza kuwa, lugha ni chombo cha mawasiliano na nyenzo muhimu ya kupata mbinu-tambuzi, maarifa, teknolojia, mitazamo na maadili. Lugha huwa chombo cha kubadilisha maadili, mielekeo na matarajio ya watu walio na utamaduni unaawatambulisha (Trudgil, 1983).

Ulimwenguni kote, lugha huchukuliwa kuwa sehemu muhimu katika maisha ya mwanadamu kwani huwa ndiyo chombo cha mawasiliano. Lugha huwawezesha watu kuwasilisha hisia zao na mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda (Crystal, 1997). Lugha huwa chombo cha kubadilisha maadili, mielekeo na matarajio ya watu walio na utamaduni unaawatambulisha (Trudgil, 1983). Dhima ya lugha ulimwenguni imeibua haja ya kuimarisha mbinu za ufundishaji wa lugha na nyenzo za kufundishia lugha (Richards na Rodgers, 2001). Mfano mzuri ni lugha ya Kiswahili ambayo imepanuka katika matumizi yake kutoka karne ya 19 hadi sasa katika Afrika mashariki na ya kati na hata ng'ambo na kuwavutia wasomi, watafiti, wanaisimu, wanajeografia na wanahistoria (Chimera, 2000).

Kwa muda mrefu lugha ya Kiswahili imechangia katika kukidhi malengo ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kijamii na elimu. Jambo hili limeipa hadhi lugha ya Kiswahili

kiasi cha kutambulika miongoni mwa lugha saba za kimataifa katika karne ya 21 (Chiragdin na Mnyampala, 1977). Kimsingi, sera ya lugha huandaliwa na wizara maalumu iliyopewa jukumu hilo. Sera ya Utamaduni ya Tanzania (1997) ambayo huelezea sera ya lugha, imeandaliwa na iliyokuwa inaitwa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Sera ya lugha ni mwongozo wa kiutekelezaji unaohakikisha kwamba lugha zilizomo katika nchi husika, zinatumika sawasawa kulingana na mipango ya nchi hiyo na pia kutambua lugha mojawapo itakayokuwa na sifa stahiki kuwa ni lugha ya kufundishia katika ngazi husika.

Rubin na Jernudd (1971) wanaifafanua sera ya lugha kuwa ni jumla ya matukio, shughuli, au hatua za wazi na fiche zinazochukuliwa na dola kwa makusudi ya kuleta au kusitisha mabadiliko katika jamii. Mekacha (2000) kwa upande wake anaidadavua sera ya lugha kama jumla ya mawazo, matamko, sheria, kanuni na taratibu zenye kuelezea taratibu za utekelezaji wa mabadiliko ya nafasi na matumizi ya lugha katika jamii. Sera ya lugha inapaswa kuzingatia na kutamka mambo ya msingi yafuatayo; namna lugha mbalimbali katika jamii zinavyopaswa kutumika kikamilifu, namna ya kujenga stadi za lugha zitakiwazo ili kukidhi mahitaji ya vipaumbele vya taifa na namna ya kutetea haki za watu, makundi ya jamii yanayotaka kujifunza na kudumisha lugha zao (Msanjila, 2009). Kutokana na mawazo hayo, tunaweza kusema kuwa sera ya lugha ni mwongozo wa kusimamia matumizi ya lugha katika jamii au nchi na serikali ndiyo yenye dhamana ya kuandaa aina ya sera inayokidhi matakwa ya jamii husika.

Kaplan na Baldauf (1997) na Mekacha (2000:126) wanaelezea kuwa madhumuni ya

sera ya lugha kuwa yanahusu:

- i. Kulinda uasili wa lugha usichafuliwe kutokana na mwingiliano wa kimsamiati kutoka lugha nyingine (kama wanavyofanya Wafaransa kulinda Kifaransa kisiharibiwe).
- ii. Kufanyia lugha mabadiliko ili kuiondolea sifa za ubaguzi wa kijinsia (kama inavyofanywa kuhusiana na lugha ya Kiitaliano huko Italia).
- iii. Kuhuisha (ua kufufua) matumizi ya lugha iliyotoweka ili iweze kutumika tena kama ilivyofanywa kuhusiana na lugha ya Kiebrania nchini Israel.
- iv. Kurekebisha lugha ili iweze kutumika katika maeneo rasmi (kama ilivyofanywa kwa lugha ya Kituruki nchini Uturuki).
- v. Kuteua na kusanifisha lugha ili iweze kutumika katika maeneo rasmi (kama ilivyofanywa kwa Kiswahili Afrika Mashariki).
- vi. Kueneza matumizi ya lugha katika maeneo na jamii ambamo ilikuwa haitumiki awali.
- vii. Kulinda lugha ambayo matumizi yake yako hatarini kutoweka.
- viii. Kupanua mfumo, kuendeleza msamiati na kusawazisha mitindo lugha.

Kwa kuzingatia madhumuni hayo, tunaweza kuyajumuisha madhumuni hayo katika makundi makuu matatu ambayo ni Kukuza, kueneza na kudumisha au kuhuisha lugha. Lugha ya kufundishia ni lugha yenye sifa za kipekee na hadhi ya juu katika nchi husika. Tunaposema lugha fulani ina hadhi ya juu, tuna maana kwamba lugha hiyo inamnufaisha mzungumzaji kijamii, kiuchumi, kielimu, kikazi na hata kisiasa (Heine, 1992). Kwa kawaida, lugha yenye hadhi ya juu kijamii hutambuliwa na kutumika na tabaka tawala katika mawasiliano rasmi ya kitaifa na kimataifa. Lugha

yenye hadhi ya juu kijamii humsaidia mzungumzaji siyo tu kupata kazi nzuri, kupata maisha bora zaidi, bali pia humsaidia mzungumzaji kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya nchi yake. Tunasema hivi kwa sababu hadhi ya lugha hupimwa kwa kuzingatia uamilifu wa lugha zenyewe katika kukidhi mahitaji na maendeleo ya kiuchumi yaliyofikiwa na jamii hizo.

Heine (1992) amezitofautisha sifa za lugha ya kufundishia na lugha za hadhi ya juu kijamii kwa kutaja sifa teule ambazo ni pamoja na kuwa zimesanifiwa na zina tumia lugha rasmi zinakuzwa na kuenezwa kwa kuwa na mipango madhubuti iliyoandaliwa katika sera ya lugha. Maeneo ya matumizi ya lugha hizi huainishwa katika sera ya lugha na ni rahisi kwa mzungumzaji kupata kazi nzuri kwa kutumia lugha hizi na lugha hizi pia hutumiwa na watu wenye nafasi za juu serikalini, katika siasa, uchumi na imani.

Besha (1999) anaeleza kwamba matumizi ya lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu licha ya kuwasaidia wanafunzi kuendeleza vipaji vyao vya ubunifu, huwa pia ndiyo njia pekee ya kuendeleza lugha hiyo. Kwa mujibu wa Msanjila (2004) lugha inayofaa kufundishia ni ile inayokidhi haja za kitaifa na kimataifa. Lugha bora ya kufundishia ni ile itumikayo katika maisha ya kila siku. Lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa kutolea elimu kwa taifa zima au sehemu ya taifa na kwa kiwango maalumu cha elimu au viwango vyote vya elimu. Hoja hiyo inaungwa mkono na Msanjila na wenziwe (2009) waliposema kwamba lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa kutolea maarifa katika mfumo wa elimu. Lugha hiyo ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa mawasiliano katika elimu ya msingi kwa umma,

kubuni na kuendeleza maarifa. Kwa mtazamo wao lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi.

Senkoro (2004) anashadidia kuwa lugha ifaayo kufundishia ni ile inayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi. Pia kwa mujibu wa Prah (2003), lugha ya kufundishia ni ile yenye athari kubwa katika mfumo wa elimu ni nyenzo itumikayo kujenga mfumo thabiti wa elimu ina nguvu na mamlaka kwa kuwa dhana kuu za elimu tayari zimo kwenye lugha hiyo ya asili, au ya karibu, kama kilivyo Kiswahili kwa Watanzania wengi. Lugha ya kufundishia ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa lolote.

Kwa mujibu wa Brock-Utne na wenzie (2005), ujuzi katika lugha ya kufundishia ni jambo muhimu kwa sababu inawezesha wanafunzi kuuliza maswali, kujadili na kubainisha mada na wenzao au mwalimu, kufikiri kwa kina namna maarifa mapya yanavyohusiana na yale waliyo nayo. Kwa upande mwingine kukosa umilisi wa lugha ya kufundishia ni kipingamizi kwa wanafunzi kuelewa jinsi ya kuunda maswali, hoja za mijadala na kufikiri kwa kina. Halikadhalika O-Saki (2003) anadai kwamba, pale walimu na wanafunzi wanapofanya kazi katika mazingira ya lugha wasiyokuwa na umilisi wake ni vigumu kuelewana na ni vigumu kwa mwanafunzi kuelewa dhana ya mada iliyofundishwa. O-saki (keshatajwa) anadai kwamba, kimsingi umilisi wa lugha ya kufundishia ni njia mojawapo ya kupitishia maarifa ya mfumo wa elimu ya jamii, kanuni za misamiati na utamaduni wa jamii husika.

Brock – utne na wenzie (2003) wanasema kwamba ususi katika lugha ya kufundisha ni jambo muhimu kwa sababu inawezesha wanafunzi kuuliza maswali, kujadili na

kubainisha mada na wenzao au mwalimu, kufikiri kwa kina namna maarifa mapya yanavyo husiana na yale yaliyonayo. Kwa sasa, Kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Kenya na Tanzania. Pamoja na kuwa kitambulisho cha utaifa wa Wakenya na Watanzania, Kiswahili hutumiwa katika mawasiliano na shughuli zote za kitaifa.

Kiswahili kama Lugha ya kufundishia nchini Tanzania. Kutangazwa kwa Azimio la Arusha mnamo mwaka 1967 ni tukio la kihistoria lililofafanua Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Kwa hivyo, ili kufanikisha elimu ya kujitegemea, suala la lugha lilihitaji kushughulikiwa na kuwekwa wazi. Mwaka huo huo wa 1967 lilianzishwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ambalo ndilo lenye jukumu la kukuza, kueneza na kuimarisha lugha. Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya kufundishia masomo ya kiwango cha elimu ya msingi mnamo mwaka 1968 (Massamba, 1989; Sewangi, 2004). Kabla ya hapo, ni madarasa manne tu ya mwanzo ya shule ya msingi ndiyo yaliyotumia Kiswahili.

Kiingereza kilitumiwa kufundishia madarasa yote ya juu (BAKITA, 2005). Baadaye, uamuzi mwingine muhimu ulifikiwa wa kutumia Kiswahili kufundishia katika vyuo vya mafunzo ya ualimu wa shule za msingi (Msanjila, 1990). Hali hii ingali ipo hadi sasa Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu (1984), Kiswahili kinatakiwa kitumike kwenye nyanja za kijamii na kisiasa, elimu ya msingi, vyuo vya ualimu wa shule za msingi na elimu ya watu wazima. Katika taasisi na vyuo vya elimu ya juu ambapo Kiswahili hufundishwa kama somo, lugha hii hutumiwa kufundisha kozi mbalimbali za isimu na fasihi.

Aidha Sera ya Elimu (2011:38) inaeleza kuwa, lugha ya kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha ya kufundishia elimu ya awali na msingi ni Kiswahili. Aidha, lugha ya Kiingereza inatumika kufundishia katika baadhi ya shule za awali na msingi. Pia, sera ya elimu na Mafunzo (2014:37) inatamka kuwa, serikali itahakikisha kuwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na nyingine za kigeni zinafundishwa kwa ufasaha na ufanisi katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini ili kuleta ufahamu na umahiri kutokana na umuhimu wa lugha hizo katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Lugha ya kiswahili imekuwa ina uwezo mkubwa wa kuweza kupewa dhima ya kufundishia shule za msingi.

Mochiwa (1979), Mekacha (1995) na (1997) wanaonyesha kwamba, watoto wengi wa vijijini wenye uelewa wa Kiswahili kama lugha ya pili umeongezeka, idadi ya watazania wanaotumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kwanza inaongezeka kwa haraka pia. Qorro (2005) anasisitiza kwamba nchi nyingi duniani ambazo hutumia lugha zake huonyesha mafanikio katika uchumi, siasa na jamii; akitoa mfano wa China inayoonyesha mfano mzuri wa kutumia lugha yake kufundishia watu wake na matokeo yake ni kuwa na maendeleo makubwa ya kiuchumi.

Kwa mujibu wa Qorro (keshatajwa) kama alivyomnukuu Rubagumya (2003), Kiswahili ni lugha inayopaswa kutumiwa katika nyanja zote za mawasiliano ya kitaifa hasa katika shule kwa kufundishia wanafunzi wa shule za msingi. Matumizi ya Kiswahili kufundishia yamesaidia kujenga saikolojia ya kujiamini na kujithamini miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia ni kuukumbatia utamaduni wa Kiafrika shuleni na kuibainisha thamani

yake kielimu na kitaaluma. Aidha, kutumia Kiswahili ni kuonesha kuwa lugha za Kiafrika zinatekeleza dhima muhimu katika ulimwengu wa kisasa. Kwa hivyo, zinapaswa kusanifishwa na kuendelezwa kwa minajili ya matumizi mapana katika medani za elimu, sayansi na teknolojia ili kuondokana na kasumba ya kuiga kikasuku mambo ya kigeni na kudharau ya kwetu.

Kwa mujibu wa wataalamu wa saikolojia, watoto wana uwezo mkubwa wa kufundishwa kitu chochote kwani akili zao hazijachafuliwa wala kujazwa mambo mengi. Imethibitika pia kuwa watoto huwa na kiwango cha juu cha ubunifu katika Nyanja mbalimbali. Ni wazi kuwa nchi zote zinazoinukia kimaendeleo, zimeendelea na zinazidi kupata ufanisi kwa kutumia lugha zao. Mifano ni kutoka nchi kama vile Japani, Uchina, Korea ya Kusini na Uswisi imethibitisha hili. Pamoja na kutumia lugha zao kuwafundishia watoto, wao wanapata ajira kimataifa, wanafaulu mitihani yao, wameendeleza nchi zao kiviwanda na huwasiliana na watu wa mataifa mengine. Kwa mujibu wa Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:1-2), ufundishaji wa somo la Kiswahili katika elimumsingi umelenga kumwezesha mwanafunzi:

- a) kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili
- b) kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali.
- c) kutumia Kiswahili kupata maarifa, stadi na mwelekeo wa kijamii, kiutamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.
- d) kukuza stadi za mawasiliano ili kumwezesha mwanafunzi kumudu maisha yake
- e) kujenga msingi bora na imara wa kujifunza kwa ajili ya elimu ya juu na kujiendeleza binafsi kwa kutumia lugha ya Kiswahili.
- f) kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Taifa.

Kwa hali hiyo, hayo ndio matarajio ya kiwango cha ufahamu wa lugha kwa wanafunzi pindi wamalizapo shule za msingi. Aidha ilikuona kama malengo hayo yamefikwa upimaji ni wa muhimu sana.

Babyegeya (1998:4) anaeleza kuwa upimaji ni mchakato wa kutafuta na kupata ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa au stadi katika kiwango fulani cha elimu na kiwango hicho hutambulishwa na kufafanuliwa katika namba hasa asilimia. Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji upimaji hujumuisha mazoezi anayoyapata mwanafunzi na kuyafanya na kwa kuangalia alama alizopata katika mazoezi au majaribio husika.

TET (2006:2) wanaeleza kuwa upimaji katika elimu ni tendo la kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amejenga uwezo, amepata maarifa au amejenga stadi tarajiwa kufuatana na malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada za masomo yaliyopo kwenye mtaala. Katika elimu, upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi hufanywa ili kujua maendeleo na hasa kujua ni kwa kiasi gani amejenga uwezo, stadi na maarifa. TET (2005:15), wanasema kuwa zipo aina zifuatazo za upimaji wa wanafunzi: Upimaji wa awali, upimaji endelevu, upimaji tatuji/gunduzi na upimaji wa mwisho/tamati. Upimaji wa awali ni upimaji ambao unapima uwezo wa mwanafunzi alionao wa kumudu kuanza kozi au mafunzo ya ngazi fulani na pia husadia kuabinisha kama mwanafunzi ana tatizo lolote linaloweza kumkwamisha katika kujifunza kwake. Upimaji huu mara nyingi hufanyika mara tuu mwanafunzi anapofika shuleni kwa mara ya kwanza kwa lengo la kuangalia na kuona ni kiwango gani mwanafunzi anaujuzi wa kuanza masomo pia itamsaidia mwalimu kuelewa mwanafunzi ana stadi zipi na anapaswa kuanzia wapi katika kujifunza.

Aina ya pili ya upimaji ambayo ni upimaji endelevu ambao hufanyika wakati wote mwalimu anapofundisha ndani na nje ya darasa. upimaji huu unasaidia kujua maendeleo ya mwanafunzi yanayochangia kuonesha nafasi yake katika mtihani wa kumaliza muhula, mwaka na kumaliza ngazi ya elimu kama vile elimu ya awali na msingi zana zinazotumika katika kufanya upimaji huu ni pamoja na mazoezi ya darasani, majaribio, orodha hakiki na mtihani mdogo (chokozo). Aina ya tatu ya upimaji ni upimaji tatuji/gunduzi, ambao ni upimaji unaobainisha matatizo waliyonayo wanafunzi na kutafuta mbinu za kuweza kuyatatua na kuweka mpango maalumu wa kuboresha ufundishaji

Upimaji wa mwisho/tamati, upimaji huu hufanyika mwisho mwa kozi au mafunzo fulani lengo lake likiwa ni kujua iwapo mwanafunzi amepata maarifa, stadi na mielekeo kwa kuzingatia Nyanja kama ilivyoorodheshwa katika muhtasari wa somo husika. Sera ya elimu na mafunzo (2014) inaelezea kuwa lengo ni Kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Na pia inatamka kuwa, Serikali itaweka mfumo wa upimaji na tathmini katika elimu na mafunzo utakaozingatia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa kila siku wa maendeleo ya mwanafunzi na mitihani ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika ya elimu na mafunzo kulingana na mitaala iliyopo katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:4), unafafanua kuwa, upimaji ni kipengele muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Kiswahili utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika elimumsingi. Upimaji huu utamwezesha mwalimu kupima umahiri wa mwanafunzi

kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali, kusikiliza, kusoma kwa ufasaha, kutafsiri, kujibu maswali ya habari, kuandika sentensi, habari fupi na hadithi kwa kuzingatia kanuni za uandishi. Aidha utamwezesha mwalimu kubaini uwezo wa wanafunzi kwa kutumia msamiati sahihi katika miktadha mbalimbali.

Kipengele ambacho utafiti huu utakishughulikia ni kile cha upimaji wa ufahamu na kutathmini ubobezi wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

1.2 Tatizo la Utafiti

Ili kufahamu kama malengo ya sera ya elimu juu ya lugha ya kufundishia yamefikwa na madhumuni ya muhtasari wa somo la kiswahili nchini yamefikwa, upimaji wa kile kilicholengwa ni wa muhimu sana. TET (2005:2-3) wanasema kuwa upimaji ni muhimu kwa kuwa, huamsha ari ya watoto kujifunza zaidi kujua maendeleo ya wanafunzi kiakili, kimwenendo, kitabia na kistadi, kumpa mwalimu mwelekeo wa kuboresha ufundishaji, kutoa taarifa ya maendeleo kwa wazazi au walezi na kutoa taarifa za maendeleo ya elimu kwa taifa. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa, upimaji katika elimu ni kitu muhimu sana, mtu anapotaka kujua maendeleo yaliyopatikana wakati wa kujifunza au kufundisha. Upimaji humuonyesha anaejifunza ni mahali gani amefanikiwa na ni mahali gani ana mapungufu. Vilevile anaefundisha anajua ni mahali gani amefanikiwa au ni wapi hajafanikiwa.

Kadiri ya Muhtasari wa Kiswahili (1996:V), baadhi ya malengo ambayo ndio dira kwa mafundisho yanayotolewa shuleni juu ya lugha ya kufundishia ni pamoja na kuwa wanafunzi wanapomaliza elimu ya msingi watakuwa ni wenye maarifa, ujuzi

na stadi za msingi za mawasiliano kusoma, kuandika, kuandika na kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali. Sera ya elimu (2014:20) inaeleza kuwa, lengo la jumla ni ‘kuwa na watanzania walioelimika na wenye maarifa na ujuzi kuweza kuchangia kwa haraka katika maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani. Vile vile sera ya elimu (2014:29) inaeleza kuwa, serikali kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha mitaala inazingatia stadi za msingi za mawasiliano, kusoma, kuandika na kuhesabu, kutafiti, kuchambua taarifa, kutafsiri, kutathimini na kutumia maarifa, uvumbuzi, ubunifu na ujasiriamali katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:2), ufundishaji wa somo la Kiswahili katika elimumsingi umelenga kumwezesha mwanafunzi, kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili, kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali na pia kutumia Kiswahili kupata maarifa, stadi na mwelekeo. Kutokana na malengo hayo ya ufundishaji kwa wanafunzi wa shule za msingi, Kwa mantiki hiyo, utafiti huu umelenga kufanya upimaji kwa wanafunzi wa shule za msingi kuona kama kweli wanaujuzi na ubobezi katika lugha ya Kiswahili hali inayopelekea wanazuoni na watafiti mbalimbali kupendekeza kuwa, kutokana na umilisi na ubobezi walionao wanafunzi, Kiswahili kitumike si tu kama lugha ya kufundishia kwa elimu ya msingi bali hata sekondari na vyuo vya kati vya elimu.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na lengo kuu na malengo mahsusi.

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kupima ufahamu wa wanafunzi katika lugha kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi.

1.3.2 Malengo Mahususi

- i) Kupima ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa shule za msingi Geita.
- ii) Kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia shule za msingi.

1.4 Maswali ya Utafiti

Majibu ya maswali ya utafiti yameongeze maarifa katika taaluma inayofanyiwa utafiti.

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Ni kwa kiwango gani wanafunzi wa shule za msingi wana ubobezi wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia ?
- b) Ni kwa kiwango gani, kiwango cha ubobezi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi kinalandana au kukinzana na sifa tarajali za ubobezi katika lugha ya kufundishia shule za msingi ?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yamekuwa na umuhimu kwa wadau wa elimu kama ifuatavyo:-

- i) Kwa upande wa walimu, utafiti huu utawasaidia kutambua kiwango cha

uelewa wa mwanafunzi kwa yale waliojifunza, kurekebisha zana za kufundishia na kujifunzia, kubaini matatizo wanayopata wanafunzi wanapojifunza na kuyatafutia ufumbuzi, kurekebisha mbinu za kufundishia na kujifunzia ili kuleta ufanisi wenye mwelekeo wa kuleta ujenzi wa maana zaidi, kurekebisha mazingira ya kujifunzi na kufundishia.

- ii) Utafiti huu utaiwezesha Serikali na watunga sera kufanya maamuzi juu ya matumizi ya lugha ya kufundishia sii tuu kwa shule za msingi pia hata kwa elimu ya sekondari
- iii) Utafiti huu utawachochea watafiti wengine watakaopenda kufanya utafiti katika uwanja wa lugha ili kuziba mapengo yaliyoachwa na utafiti huu.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umehusu upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi Tanzania. Utafiti huu ulilenga kuona uwezo wa umilisi na ubobezi walionao wanafunzi katika lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia kwa shule za msingi zilizo katika wilaya ya Geita vijijini. Ingawa ufundishaji na ujifunzaji hufanyika katika stadi mbalimbali, Katika utafiti huu upimaji ili kujua umilisi na ubobezi walionao wanafunzi wa darasa la saba utafiti huu, utafanyika katika mada za msamiati, aina za maneno na matumizi ya maneno katika nyakati mbalimbali. Kwa upande wa msamiati, kwamba ni kwa kiasi gani wanafunzi wana ufahamu wa maneno mbalimbali na utumizi wake katika sentensi, katika aina za maneno ni kwa kiasi gani wana uwezo wa kutaja na kubaini aina za maneno katika sentensi na Matumizi ya njeo katika nyakati mbalimbali.

1.7 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza vipengele mbalimbali vya utafiti ambavyo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti ambayo ni lengo kuu na lengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na hitimisho.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii imetalii na kutathimini mapitio ya kinadharia na ya kazi tangulizi. Marejeleo ya vitabu na machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti huu yamehusika. Sura hii imeonesha mtazamo wa wataalam mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada hii ya utafiti. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi, inafuatiwa na sehemu ya pili, ambayo ni mapitio ya kitaaluma na ya kazi tangulizi na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Aidha, pengo la utafiti na kiunzi cha nadharia vimeonyeshwa ndani ya sehemu hii.

2.2 Dhana ya Lugha, Uamiliaji Lugha na Ujifunzaji Lugha

Kabla ya kuongelea juu ya lugha fulani, ni jambo la muhimu kuelewa kwanza fasili ya lugha. Wataalam mbalimbali wameielezea lugha kwa namna zinazotofautiana kwa kiasi kidogo sana. Wafuatao ni miongoni mwa wataalamu hao. Habwe na Karanja (2004), wakiinukuu TUKI (1990), wanasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu katika jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Masamba na wenzake (2009), wanaeleza kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao. Hivyo basi, kulingana na maelezo ya wataalam hao, lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo hutumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana kwa madhumuni ya mawasiliano miongoni mwa jamii hiyo.

Binadamu anapozaliwa anakuwa na bohari la sauti mbalimbali zisizo na maana yoyote. Chomsky (1957) anasema kwamba, binadamu huzaliwa akiwa na uwezo wa

lugha. yaani kwenye ubongo wake ana mfumo ambao huzaliwa nao kwa ajili ya kujifunza lugha. Ana kiendea kazi kisichoshikika kinachoitwa LAD (Kifaa cha upataji lugha). Mara anapoanza kuishi katika jamii ndipo huanza kuibua sauti hizo katika mazingira bila mwenyewe kutarajia na kuanza kuzitafutia maana.

Wataalam mbalimbali wameongelea juu ya uamiliaji lugha. Krashen na Tracy (1983) wanasema kuwa uamiliaji lugha ni mchakato unaotokea katika nafsi iliyofichika akilini mwa mtu ambayo ndiyo imuongozayo kuongea au kuandika kwa urahisi. Hivyo wao wanaona kuwa uamiliaji hujitokeza kwa mtu katika hali ya ung'amuzi bwete pasipo mhusika mwenyewe kujitambua. Jean (1992:123) anasema kuwa katika uamiliaji lugha watoto wachanga wanakuwa makini katika lugha tangu wanapozaliwa. Wanaanza kutoa maneno yanayotambulika katika kipindi cha miezi 12 hadi 15 na kuanza kuyaunganisha maneno hayo kuanzia miezi 18. Anaendelea kusema kuwa watoto wote wasio na matatizo ya kimaumbile na baadhi wenye matatizo wataanza kuongea ikiwa watasikia lugha ikizungumzwa katika mazingira waliyomo.

Massamba (2004) anasema kuwa ujifunzaji lugha ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kuijua na kuitumia lugha fulani. Mtu yeyote ana uwezo wa kujifunza lugha na kuifahamu ikiwa tu atakuwa na akili timamu pamoja na ala sauti zote zinazohusiana na ujifunzaji lugha kikubwa tu ziwe hazijaathiriwa au kuathirika. Kwa mujibu wa Chomsky (1976:29), kama alivyonukuliwa na Ellis (1994:430), sarufi majumui ni mfumo wa kanuni na sheria ambazo ni msingi wa lugha za binadamu. Msingi wa nadharia hii ni kwamba binadamu anapozaliwa anakuwa na maarifa asilia ambayo humsaidia katika ujifunzaji wa lugha. Maarifa haya hupatikana pale tu

binadamu anapozaliwa kwani huwa na kifaa cha uamiliaji lugha ambacho kinakuwa na kanuni majumui na kanuni badilifu ambazo hukutana na tajiriba (uwezo wa jamii katika lugha) na kusababisha uamiliaji lugha kutokea.

2.3 Lugha ya Kufundishia

Lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa na mwalimu kufundishia wanafunzi (Zhou na Sun 2004). Aidha, lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa kutolea elimu kwa taifa zima au sehemu ya taifa na kwa kiwango maalum cha elimu au kwa viwango vyote vya elimu. Msanjila na wenzie (2009) wanadai kwamba lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa kutolea maarifa katika mfumo wa elimu. Lugha hiyo ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa mawasiliano katika elimu na kuwasilisha stadi na maarifa ya msingi kwa umma, kubuni na kuendeleza maarifa. Msanjila na wenzie (wameshatajwa) kadhalika wanaendelea kudai kwamba, lugha ya kufundishia huwa ni chombo cha kuwapa watu uwezo na nguvu kiutamaduni na kisayansi.

Aidha, Msanjila na wenzake (wameshatajwa) wanaendelea kudai kwamba lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugrunduzi. Msanjila na wenzie (2009) wanasema kwamba lugha ya kufundishia ni lugha inayotumika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu wa nchi. Matumizi ya lugha kama lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu, zaidi ya kuwasaidia wanaojifunza kuendeleza vipaji vyao vya ubunifu, huwa pia ndiyo njia ya kuendeleza lugha hiyo ili kukabili taaluma za sayansi na teknolojia.

Naye Qorro (2006) anatoa hoja kwamba lugha ya kufundishia ni chombo cha kupitishia elimu kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi na miongoni mwa wanafunzi wenyewe. Hali kadhalika, Qorro (2005) anafafanua kwamba pale wanafunzi wanaposhindwa kuongea lugha ya kufundishia hakika hawataweza kujifunza. Mtaalamu huyo aliendelea kudai kwamba, lugha yenye ufanisi na ya kuleta matokeo yanayotakiwa ni ile tu inayofahamika vizuri kwa walimu na wanafunzi. Mambo yanayochangia wanafunzi kupata maarifa katika ujifunzaji wao ni kufundishwa kwa kutumia lugha waliyo na umilisi wake.

Kwa mujibu wa Mekacha (2000), lugha ni nyenzo inayoweza binadamu kufikiri, kuwasiliana, kuhifadhi na kurithisha maarifa. Lugha ni nyenzo muhimu sana katika kufikiri. Kila mara binadamu anapotumia lugha hufikiri kwanza, anapotaka kusema lolote hufikiria kwanza jambo la kusema na namna ya kulisema ili ujumbe aliokusudia kuuwasilisha ufikishwe kwa msikilizaji bila utata. Kwa hiyo basi haiwezekani watu kufikiri bila kutumia lugha. Mtu anapofundishwa katika lugha anayoifahamu vizuri huelewa anachofundishwa na huweza kueleza vyema alichojifunza kwa maneno yake na hata huweza kuwa na ugunduzi kwa vile hufikiria kwa kutumia lugha anayoielewa.

Vilevile Msanjila na wenzake (2011) wanasema kuwa lugha ya kufundishia inapoteuliwa visivyo, huwa kunajitokeza vikwazo vingi ambavyo huathiri ufanisi katika kutoa, kubuni na kuendeleza maarifa. Vikwazo hivyo ni wajifunzaji kuwa na mtazamo wa kutoipenda lugha hiyo, kuondoa juhudi ya kuijua na kuitumia, hivyo kukwamisha michakato ya ujenzi na utoaji wa maarifa muhimu kwa maendeleo ya jamii. Hivyo basi, ili mwanafunzi apate maarifa na uwezo wa kujitambua na

kung'amua kile kilichofundishwa na mwalimu wake lazima awe na umilisi wa lugha ya kufundishia.

Rubagumya (2003) anadai kwamba, ufundishaji unaotumia lugha inayofahamika baina ya walimu na wanafunzi huleta ufanisi wa kutosha kwa sababu wanafunzi watajua jinsi ya kutumia maarifa ya kidhanifu katika taarifa mpya. Rubagumya (keshatajwa) anaenelea kudai kwamba, lugha inapokuwa ni ile iliyozoeleka kwa wanafunzi na ambayo walimu wanaimudu vyema huuleta uelewa mzuri wa dhana ya somo linalofundishwa. Kwa mujibu wa Puja (2003), ujuzi wa lugha ya kufundishia ni kigezo muhimu cha kufanya vizuri shuleni. Naye Mekacha (2000) anadai kuwa, watu hufikiri katika lugha na lugha hutumika katika kufikiri, lugha ndiyo nyenzo ya kuwasilisha na kuweka wazi fikra na mawazo. Kutokana na hali hii ni wazi kuwa lugha na kufikiri ni mambo yanayofungamana. Aidha, Mekacha (amesha tajwa) anasema: Lugha na kufikiri ni mambo yaliyofungamana mno kiasi kwamba haiwezekani.

Kujadili mojawapo bila kulihusisha na jingine, kusema kuna hudumia fikra na Fikra hujibainisha katika kusema (uk 3). Kwa hivyo, lugha ya kufundishia inatakiwa iwe ndiyo inayowezesha mwanafunzi kufikiri na kuamua kipi akiseme kwa wakati ulio sahihi. Prah (2003) anaeleza kwamba, lugha ya kwanza ikitumika kama lugha ya kufundishia huwezesha watu kujiamini. Kwa hali hiyo, lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi. Prah (amesha tajwa) anaendelea kudai kwamba, lugha ya kufundishia ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa elimu na ndiyo lugha

inayotumiwa kuwasilisha stadi na maarifa ya msingi ya umma na ndiyo ya kuimarisha ubunifu na kuendeleza maarifa ya wajifunzaji. Kwa hali hii basi, huwa ndiyo lugha ya kulimbikiza na kuhifadhi maarifa. Naye Tikolo (2012) anatoa hoja kwamba, ufahamu wa wanafunzi wa lugha aliyoizoea wakati wa kukua kwake inaweza kuwa ndiyo msingi wa ujifunzaji mzuri wa baadaye, pale anapounganisha na ujuzi wa mwalimu wake.

Kwa jumla, lugha ya kufundishia inapaswa kuwa ni ile inayotumiwa na watu wengi katika mawasiliano yao ya kila siku kama ilivyo kwa Kiswahili. Ikitumika lugha hiyo itafungua milango ya kupitishia maarifa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi na kwenda kutumika katika jamii na huwa ndicho chombo cha kumwezesha mwanafunzi kung'amua, kueleza na kutekeleza hisia zake za ndani kwa kile kinachomfikia au kinachotoka moyoni mwake (Qorro, 2000). UNESCO (1953) kwa upande wake inaona kuwa lugha za jamii ni bora katika kufundishia kuliko lugha zote za kigeni. Inabainisha sababu tatu kama ifuatavyo, moja, lugha ya jamii ni mfumo wa dhana zenye maana kwao ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kujielezeka na kueleweka. Mbili, lugha ya mtu ni njia ya kujinasibisha na kwao. Tatu ni sababu ya kielimu ambayo kwayo mwanafunzi hujifunza haraka kupitia lugha anayoielewa vema kuliko lugha ngeni.

2.4 Lugha Rasmi za Kufundishia na Kujifunzia Tanzania

Mchakato wa kutafuta lugha rasmi ya kufundishia na kujifunzia nchini Tanzania unaweza kutazamwa kihistoria katika vipindi viwili ambavyo ni kabla na baada ya uhuru. Katika utawala wa Wajerumani (1887- 1918) matumizi ya Kiswahili

yalihimizwa (Gottneid, 1977). Walitumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi (Whiteley, 1969). Utawala wa Waingereza (1919 -1961) uliendeleza Kiswahili kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la nne. Kuanzia darasa la tano, Kiingereza kilitumika kufundishia masomo yote na Kiswahili kikabaki kuwa somo la lazima katika miaka minne (4) ya shule za kati na miaka minne (4) mingine kwa elimu ya sekondari. Jambo la msingi lililofanywa na utawala wa Waingereza ni kughushi lugha ya Kiswahili. Kitendo hicho kilibadilisha Kiswahili fasaha kuwa Kiswahili kipya cha shule (kisanifu) na kupotosha matumizi ya lugha asilia inayojidhihirisha kwenye lahaja za Kiswahili mfano kimtang'ata kitumbatu (Sengo, 2017).

Wakati wa uhuru, kati ya miaka ya 1967 hadi 1987, elimu ya Tanzania ilifuata itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea. Mabadiliko ya itikadi toka ubepari kuwa ya Ujamaa kuliambatana na mabadiliko makubwa katika mfumo wa elimu. Katika utekelezaji wa itikadi hiyo katika mfumo wa elimu, kulianzishwa elimu ya kujitegemea. Kiswahili kilifanywa kuwa lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi kwa sababu ilikuwa inazungumzwa na watu wengi. Lengo la elimu ya kujitegemea lilikuwa ni kuwawezesha wanafunzi kujitegemea baada ya kumaliza elimu ya msingi. Ukweli wa lengo hilo ulifahamika na wahitimu wote wa shule za kati.

Hatua hiyo ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi za shule za msingi ilikuwa ndani ya mpango mkubwa wa utekelezaji wa Kiswahili kukifanya kuwa lugha ya kufundishia ngazi zote za elimu (Brock-Utne, 2000). Hayo yalitokana na tamko rasmi la aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati huo, Mheshimiwa Rashid

Mfaume Kawawa. Alikusudia kufanya Kiswahili kitumike pote na kwa wote ikiwa na maana kwa Watanzania na wageni (Sengo, 2017). Brock- Utne (2000) anadai kuwa mwaka 1969 Wizara ya Elimu ya Taifa ilitoa waraka kwa wakuu wote wa shule za sekondari, ikiwataka kuanza utekelezaji wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia. Waraka huo ulipendekeza kuwa somo la siasa linapaswa kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili kuanzia mwaka 1969/1970, Sayansi Kimu 1970 /1971, Historia, jiografiaa, Biolojia, kilimo na Hisabati miaka 1971 na 1972 (Bhaiji, 1976).

Bhaiji (keshatajwa) anaendelea kubainisha kuwa wakuza mitala walishaanza kutarijamu na kukusanya istilahi za masomo ya Sayansi na Hisabati. Katika kipindi hicho baadhi ya shule za Sekondari zilikwishapata kijitabu chenye istilahi za Hisabati katika lugha ya Kiswahili. Miaka ya mwishoni mwa 1970 ilishuhudia kuibuka kwa mjadala mkali kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia ngazi zote za elimu. Mjadala huo umedumu hadi leo. Kutokana na mjadala huo, maoni ya kufuja wazo la kuitumia lugha ya kufundishia nchini Tanzania yaligawanyika katika pande mbili: wale waliokubali kuwa Kiswahili kitumike kufundishia ngazi zote za elimu na wale waliopinga na kushadidia kukifanya Kiingereza kiendeleo kutumika katika ngazi zote za elimu.

Aidha, Tume ya Rais ya mwaka 1982 ilipendekeza Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu nchini Tanzania (United Republic of Tanzania, 1984). Kuanzia, miaka ya 1987, nchi ilianzisha sera ya soko huru. Sera hiyo iliambatana na ubinafsishaji wa njia kuu za uzalishaji mali. Mabadiliko hayo

yaliathiri mfumo wa elimu pia. Miaka ya 1990 ilishuhudia ongezeko la shule binafsi za Msingi na za Sekondari. Katika kipindi hicho serikali ilipitisha marekebisho ya kanuni ya Elimu ya mwaka 1995. Shule binafsi za msingi ziliruhusiwa kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia ilihali shule za msingi za serikali zikiendelea kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia. Hali Sera ya Utamaduni (1997) inatamka kwamba mipango itafanywa ya kukiwezesha Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia katika Elimu na Mafunzo ya ngazi zote. Tofauti na zilizotangulia Sera ya Elimu na mafunzo (2014) inatamka kuwa lugha ya Taifa Kiswahili itatumika kufundishia ngazi zote za Elimu na Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hiyo kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa.

2.5 Dhana ya Upimaji

Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:1-2) unaeleza kuwa, ufundishaji wa somo la Kiswahili katika elimu ya msingi umelenga kumwezesha mwanafunzi, kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali. Kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Taifa. Kwa maana hiyo, hayo ndio matarajio ya kiwango cha ufahamu wa lugha kwa wanafunzi pindi wamalizapo shule za msingi. Aidha ilikuona kama malengo hayo yamefikwa upimaji ni wa muhimu sana. Nayo TET (2006:2), katika kitabu cha mwongozo wa tathimini na upimaji, inaeleza kuwa upimaji katika elimu ni tendo la kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amejenga uwezo, amepata maarifa au amejenga stadi tarajiwa kufuatana na malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada za masomo yaliyopo kwenye mtaala. Katika elimu, upimaji wa maendeleo ya

mwanafunzi hufanywa ili kujua maendeleo na hasa kujua ni kwa kiasi gani amejenga uwezo, stadi na maarifa.

Sera ya elimu na mafunzo (2014) inaelezea kuwa lengo ni Kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Na pia inatamka kuwa, Serikali itaweka mfumo wa upimaji na tathmini katika elimu na mafunzo utakaozingatia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa kila siku wa maendeleo ya mwanafunzi na mitihani ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika ya elimu na mafunzo kulingana na mitaala iliyopo katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:4), unafafanua kuwa, upimaji ni kipengele muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Kiswahili utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika elimumsingi. Upimaji huu utamwezesha mwalimu kupima umahiri wa mwanafunzi kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali, kusikiliza, kusoma kwa ufasaha, kutafsiri, kujibu maswali ya habari, kuandika sentensi, habari fupi na hadithi kwa kuzingatia kanuni za uandishi. Aidha utamwezesha mwalimu kubaini uwezo wa wanafunzi kwa kutumia msamiati sahihi katika miktadha mbalimbali. Upimaji ni utaratibu wa kujua uwezo, maarifa au utendaji wa wanafunzi yale anayojua na yale ambayo hayajui ambayo tayari amefundishwa. Rivers (1968) anasema utaratibu huo unaonyesha yale asiyoyajua mwanafunzi na yale ambayo anayajua. Bachman na Palner (1996) wanaeleza kuwa upimaji (majaribio bora) uzingatie vipimo vya ubora vifuatavyo uaminikaji, uthibitikaji, uhalisia na uhusianifu ili yalete matokeo yaliyokusudiwa na utekelezaji mzuri.

Katika madarasa ya Kiswahili upimaji huwa ama wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi, kuchagua jibu sahihi kati ya majibu kadhaa, kuteua jibu lililo kweli au lisilo kweli au kuoainisha majibu. Mwanafunzi anatarajiwa kuonesha amejifunza mada husika kwa kiwango gani pamoja na utendaji wake wa lugha. Muhtasari wa somo la Kiswahili (2005:96) unaeleza kuwa wanafunzi katika makundi wabainishe aina za maneno na dhima zao mbalimbali katika sentensi na pia waweze kuunda sentensi kwa kutumia aina mbalimbali za maneno.

Haya ni malengo ambayo yanapaswa yafikiwe baada ya kuwa mwanafunzi amemaliza kufundishwa mada hiyo, lakini pia katika muhtasari huo wa somo la Kiswahili (2005:98), wanafunzi wanatarajiwa kuweza kujibu maswali ya ufahamu, kuonesha uelewa na matumizi ya msamiati kwa ufasaha. Na pia muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:56) unaoonesha kuwa mwanafunzi anataegemewa kuwa na uwezo wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowakilishwa katika matini mbalimbali na kuweza kubaini maneno katika matini na kuelezea maana zake.

2.6 Mapitio ya kazi Tangulizi

Criper na Dodd (1984) walifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari. Katika utafiti huo wataalamu hao walichunguza ujuzi wa lugha ya Kiingereza walionao walimu na wanafunzi katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari nchini Tanzania. Ili kupata matokeo ya kile walichokuwa wakikichunguza, wataalamu hao walitoa majaribio kwa wanafunzi elfu mbili mia nne na kumi kutoka ngazi zote za elimu. Matokeo ya majaribio hayo

yaliwafanya wataalamu hao kugundua kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari siyo njia sahihi ya kutolea elimu katika ngazi hizo. Kueleweka kwa lugha ya Kiingereza kuko chini sana takribani katika shule zote zilizofanyiwa utafiti huo. Ni dhahiri kwamba matumizi ya Kiingereza yanafanya kujifunza kuwa kugumu. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha asilimia kumi ya wanafunzi wa kidato cha nne waliofanyiwa utafiti walikuwa na uwezo mdogo wa kuelewa kitu chochote kilichofundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Pili, asilimia ishirini ya wanachuo waliokuwa katika kundi lilopimwa walikuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa vitabu vya taaluma mbalimbali walizokuwa wanasomea. Msingi mzuri ama mbovu wa lugha ya Kiingereza walio nao wanachuo wa vyuo vya kati una athari kubwa katika kujifunza na kufaulu kwao katika fani wanazosomea. Kimsingi, hujifunza lakini ufanisi haujitokezi katika mazingira ambamo wanachuo hao hawaimudu hiyo lugha ya kujifunzia ambayo ndiyo nyenzo ya kufanikishia mawasiliano katika tendo la kufundisha na kujifunza.

Msanjila (1986) alichunguza hali ya ufundishaji kwa Kiswahili katika vyuo vya ualimu. Katika uchunguzi wake alibaini kwamba licha ya kuwapo kwa istilahi za kutosheleza ufundishaji wa Kiswahili, bado walimu hawazitumii katika kufundishia kwa kuwa walimu hao walipata mafunzo yao kwa lugha ya Kiingereza. Isitoshe, walimu hao hawakuwa na marejeleo ya vitabu vya Kiswahili. Kutokana na matokeo ya uchunguzi huo, alipendekeza Kiswahili kifanywe lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na vyuo vya juu ili kukiwezesha Kiswahili kuimarika na kueneza istilahi zake na kufikisha maarifa yanayotakiwa kwa jamii. Rubagumya (1991) alichunguza utumiaji wa lugha mbili katika shule za sekondari. Kutokana na utafiti

huo, mtaalamu huyo aligundua kwamba walimu walitumia lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza katika ufundishaji ili kuwezesha maelewano yenye manufaa baina ya walimu na wanafunzi. Hii ilitokana sera iliyomlazimisha mwalimu kufundisha kwa Kiingereza ili kuwatayarisha wanafunzi kwa ajili ya mitihani inayotungwa kwa lugha hiyo. Kwa kuwa wanafunzi wanao ujuzi kidogo wa lugha ya Kiingereza, huwalazimu walimu kukiuka matakwa ya sera ya kutumia lugha ya Kiingereza na badala yake hufundisha kwa lugha ya Kiswahili au kufafanua istilahi za Kiingereza kwa Kiswahili ili kuwapa hayo maarifa wanafunzi wao.

Pasipo kufanya hivyo, ni wazi kuwa wanafunzi hawataelewa kile wanachofundishwa. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa tatizo la kutomudu lugha ya Kiingereza si la wanafunzi tu, bali hata baadhi ya walimu wanapata shida kufundisha kwa Kiingereza. Watafiti wa LOITASA (2005), walifanya utafiti kuhusu lugha za kufundishia na kujifunzia nchini Tanzania na Afrika ya Kusini. Matokeo ya utafiti yalionesha wazi kuwa matumizi ya Kiswahili katika kufundishia siyo tu yanaimarisha kujifunza na kufundisha kwa ufanisi zaidi bali pia yana manufaa kwa jamii nzima ya kitanzania. Aidha, utafiti huo ulionesha waziwazi kuwa Kiswahili nchini Tanzania ndiyo lugha inayofahamika na kutumika katika mawasiliano mapana.

Kwa hiyo, mradi wa LOITASA uliipendekeze lugha ya Kiswahili itumike katika kufundishia elimu ya shule za sekondari hadi chuo kikuu. Matokeo ya utafiti wa mradi wa LOITASA yamedhihirisha kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu hauna budi kupatiwa ufumbuzi. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Qorro na Brock-Utne (2006) nchini Tanzania kuhusu matumizi ya lugha ya

Kiingereza katika kufundishia shule za sekondari, ulibaini kuwa wanafunzi wengi na walimu wao wana matatizo katika matumizi ya lugha ya hiyo. Wanafunzi wachache sana huweza kushiriki katika tendo la kujifunza huku walio wengi wakishindwa kushiriki. Kujifunza na kufundisha kunaweza kuwa na mafanikio pale tu, walimu na wanafunzi wanapomudu kutumia lugha ya kufundishia kwa sababu ufundishaji ni mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi.

Peterson (2006) alichunguza matumizi ya lugha ya asili ya Kiafrika kama lugha ya kufundishia katika chuo kikuu kwa kuzingatia hoja ya kuanzishwa kwa idara ya Kiswahili, mkakati unaotumiwa na idara hiyo pamoja na viwango ambavyo huwafanya walimu na wanachuo wajisikie vizuri au vibaya katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa wanachuo wote waliohojiwa walikiri kuwa wanayaelewa mafunzo yaliyotolewa kwa Kiswahili kwa vizuri zaidi kuliko yale yatolewayo kwa lugha ya Kiingereza. Sababu kubwa zilizotolewa na wanachuo ni kwamba Kiswahili ni lugha ya kwanza au ya pili kwa walio wengi, ni lugha wanayoitumia nje ya darasa na ambayo hukumbana nayo katika maisha yao ya kila siku sehemu mbalimbali kama vile sokoni, nyumbani, kanisani, msikitini na hata shuleni.

Wanachuo waliohojiwa walibainisha kuwa Kiingereza kinapotumika kama lugha ya kufundishia wao hujifunza kwa kiwango kidogo sana. Sababu walizozitoa ni: kutoelewa miundo ya tungo za Kiingereza, tafauti iliyopo baina ya maandishi na matamshi, baadhi ya vitabu huwa na lugha ngumu kueleweka kwa wanachuo na maneno mengi ya Kiingereza hawayaelewi kutokana na tafauti za kiutamaduni na

Kifalsafa zilizopo. Kwa upande wa walimu (Wahadhiri) waliohojiwa katika utafiti huo, walikiri kuwa Kiswahili kinafaa kuwa lugha ya kufundishia kwa sababu ni lugha inayofahamika kwa wanachuo. Kufahamika huko huwasaidia kufahamu vizuri dhana za somo pamoja na wepesi wa kujieleza kwa uhuru zaidi kwa kutumia lugha hiyo.

Peterson (keshatajwa) aliendelea kubainisha kwa kusema kuwa kuamua kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya juu haina maana kuwa vitabu vyote sharti vitarijuniwe kwa Kiswahili. Anahitimisha utafiti wake kwa kupendekeza kuwa Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itumike kama mfano wa kuigwa katika kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia kozi zake zote.

Mlama na Matteredu (1978) walifanya utafiti juu ya lugha kufundishia vyuo vya juu, katika utafiti wao huo walitoa mapendekezo mbalimbali miongoni mwayo ni lile pendekezo la kuwa Kiswahili kitumiwe kufundishia katika elimu ya juu ili kutatua matatizo yanayosababishwa na matumizi ya kiingereza na vilivile kuikuza na kuimarisha lugha ya Kiswahili kuifanya iwe lugha ya kitaalamu. Tafiti zingine zilizokwisha fanywa kama vile Kamugisha na Mateng'e (2014) zilijikita zaidi kutafuta ulinganifu wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu.

Yoradi (2013) alifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu shule za sekondari na vyuo vya ualimu. Katika utafiti huo, mtafiti alifanya majaribio ya kufundisha somo la Biolojia kwa wanafunzi wa kidato cha I, II na III kwa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa mada alizozichagua kisha

akatoa mtihani au majaribio ya kuwapima wanafunzi hao. Matokeo ya majaribio hayo, yalionesha kuwa wanafunzi walijifunza na kuelewa vizuri zaidi na kufaulu mitihani ya somo hilo iliyotungwa kwa lugha ya Kiswahili. Hiyo ilidhihirisha maudhui ya somo la Biolojia yalieleweka vizuri zaidi kwa kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili kuliko kwa lugha ya Kiingereza. Matokeo ya Utafiti huo yalibainisha kuwa:

- i. Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka vizuri zaidi katika kufundishia na kujifunzia elimu shuleni na vyuoni.
- ii. Wanafunzi wengi hawaelewi lugha ya Kiingereza inapotumiwa kama lugha ya kufundishia.

Huwafanya wanafunzi wasiweze kupata elimu ambayo wangeipata kwa manufaa ya kuliendeleza taifa. Katika Hali halisi nchini Tanzania inaonesha kwamba Kiswahili kinatumika katika sekta mbalimbali kama vile katika mawasiliano, biashara, katika shughuli za kiutawala, ofisini, katika mahakama za mwanzo, bungeni, katika vyombo vya habari katika utekelezaji wa sheria na sera mbalimbali, katika shughuli za kisiasa, katika shule za msingi, vyuo vya elimu vinavyotoa elimu kwa ngazi ya cheti na elimu ya watu wazima na jamii kwa ujumla.

Hivyo lugha ya Kiswahili inatumika sana nchini Tanzania kama asemavyo Mekacha (2000), Kiswahili ndiyo lugha pekee inayotumika karibu katika kila nyanja ya matumizi ya lugha. Hali hii ndiyo inayofanya utafiti huu kufanya upimaji wa ufahamu walionao wanafunzi katika lugha ya Kiswahili na pia kuona ubobezi walionao wanafunzi.

2.7 Kiunzi cha Nadharia

Kwa kuwa nadharia ni dira na mwongozo, utafiti huu umeongozwa na nadharia moja ambayo ni Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) Nadharia hii ilitumika katika kuchambua malengo mahususi yote ya utafiti. Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) ilihusika katika uchanganuzi wa data zinazohusiana na umilisi wa lugha ya kiswahili katika vipengele vyote vilivyopimwa kwani nadharia hii inatoa ufafanuzi juu ya mjua lugha awe na uwezo wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, othografia, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha lazima awe na uwezo wa kiutendaji katika lugha husika yaani awe na uwezo wa kutumia lugha ile katika miktadha tofauti ya kijamii kwa usahihi. Hivyo ni dhahiri kuwa nadharia hii inao uwezo na ubora toshelevu wa kuvichanganua na kuvifafanua vipengele vyote vilivyopimwa.

2.7.1 Nadharia ya Umilisi Wa Mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981).

Katika muundo wa Canale na Swain, umilisi kamili unaundwa na maarifa ya lugha ya mazungumzo na lugha ya ishara katika mkakati wa mawasiliano ambao hutumika kufidia mawasiliano yaliyovunjika kutokana na kutoweka na umilisi kamili katika kipengele kimoja au zaidi vya umilisi wa lugha. Mikakati hii hujumuisha kufupisha habari / taarifa kwa kutumia maneno ya mzungumzaji mwenyewe, kurudiarudia, kuacha baadhi ya maneno kudondosha maneno, sarufi / maana, kuhisi kubadilika kwa lahaja na aina ya uzungumzaji, kuboresha ujumbe na kadhalika.

Kulingana na Canale na Swain (1980, 1981), ili mzungumzaji awe na umilisi wa mawasiliano wa lugha, anahitajika kuwa na mbinu za kimazungumzo na zisizo za kimazungumzo za kuhakikisha kuwa mawasiliano hayavunjiki kwa vile labda ana upungufu katika vipengele vile vingine vya umilisi wa mawasiliano kama kile cha kiisimu. Mzungumzaji lazima afahamu mbinu anazoweza kutumia ili mawasiliano yasivunjike kama vile kurudia rudia jambo, kutumia maelezo wakati amekosa neno la dhana fulani, kukwepa kutumia maneno asioyafahamu vyema kati ya mbinu nyingine”. Mzungumzaji lazima afahamu matumizi ya ishara mbali mbali anazoweza kutumia kuhakikisha kuwa mawasiliano hayavunjiki.

Kwa mujibu wa Canale na Swain (1980,1981) na Canale (1984) vipengele vya umilisi wa mawasiliano viko vinne ambavyo ni:-

- i. Umilisi wa kiisimu.
- ii. Umilisi wa kiisimujamii.
- iii. Umilisi wa mbinu za mawasiliano.
- iv. Umilisi wa uchanganuzi usemi.

Katika umilisi wa kiisimu kwa mzungumzaji, ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo. Katika Muundo wa Canale na Swain (1980, 1981) ujuzi wa kisarufi ulifasiriwa zaidi kwa kuzingatia mawazo ya Chomsky (1965) juu ya dhana ya umilisi wa lugha. Umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, othografia, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za

lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha lazima awe na uwezo wa kiutendaji katika lugha husika yaani awe na uwezo wa kutumia lugha ile katika miktadha tofauti ya kijamii kwa usahihi.

Chomsky (1957), anaeleza kuwa, mtu anapojifunza lugha huanzia na umilisi (ujuzi) na anaendelea kudai kuwa kwa kiasi kikubwa umilisi wanaokuwa nao wazawa wa lugha moja hufanana na hii ndiyo inayowafanya waelewane katika mazungumzo yao kwamba mzungumzaaji anasema kile anachotaka kusema na msikilizaji anaelewa kile kilichosemwa na mzungumzaji lugha moja hufanana na hii ndiyo inayowafanya waelewane katika mazungumzo yao kwamba mzungumzaaji anasema kile anachotaka kusema na msikilizaji anaelewa kile kilichosemwa na mzungumzaji.

Mambo mhimu kwa mzawa wa lugha kuwa nayo ili awe milifu wa lugha.

Umilisi kama dhana mojawapo ya msingi ina ulazima kwa mzawa wa lugha kuwa nayo kutokana na sababu kuwa: Humsaidia kujua miundo na aina mbalimbali za sentensi katika lugha yake, kutambua sentensi sahihi na ambazo sio sahihi, zikiwa zinaandikwa au kuzungumzwa, humsaidia kutunga sentensi zenye urefu wowote , humsaidia kutambua sentensi zenye utata na Vile vile humsaidia kutambua sentensi zenye maana sawa na sentensi zenye maana na zile zisizo na maana.

Kwa kifupi, umilisi wa kiisimu ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria hizi za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo. Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain, kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Nadharia hii ya umilisi wa

mawasiliano ya Canale na Swain itaongoza uchambuzi wa malengo yote ya utafiti huu na inatuwezesha kupima uwezo walio nao wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Na inajitosheleza katika kupima ubobezi walionao wanafunzi wa shule za msingi katika lugha ya kiswahili na pia kutathimini ubobezi waliona wanafunzi dhidi ya sifa tarajali za lugha ya kufundishia na kuchambua vipengele vyote vilivyofanyiwa upimaji kwani humsaidia kujua miundo na aina mbalimbali za sentensi katika lugha husika, kutambua sentensi sahihi na wowote , humsaidia kutambua sentensi zenye utata na Vile vile humsaidia kutambua sentensi zenye maana sawa ambazo sio sahihi, zikiwa zinaandikwa au kuzungumzwa, husaidia kutunga sentensi zenye urefu na sentensi zenye maana na zile zisizo na maana. Mtafiti ametumia nadharia hii katika kuangalia jinsi wanafunzi wanavyoweza kufuata sheria za lugha, yaani uwezo wa mzungumzaji wa kuzifahamu vyema sheria za lugha.

2.8 Pengo la Utafiti

Kulingana utalii wa kazi tangulizi, tumebaini kuwa suala la lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu Tanzania limeshughulikiwa kwa mitazamo, na kwa nyakati tofauti. Kwa mfano, Yoradi (2013) alifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu shule za sekondari na vyuo vya ualimu, vile vile Peterson (2006) alichunguza matumizi ya lugha ya asili ya Kiafrika kama lugha ya kufundishia katika chuo kikuu kwa kuzingatia hoja ya kuanzishwa kwa idara ya Kiswahili. Aidha Rubagumya (1991) alichunguza utumiaji wa lugha mbili katika shule za sekondari pia Msanjila (1986) alichunguza hali ya ufundishaji kwa Kiswahili katika vyuo vya ualimu. Kwa jumla hakuna tafiti ziliokwishafanyika za upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi. Kwa

mantiki hiyo, utafiti huu umelenga kufanya upimaji kwa wanafunzi wa shule za msingi kuona ubobezi walionao katika lugha ya Kiswahili.

2.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeona mapitio mbalimbali ya kitaaluma na ya kazi tangulizi. Sura hii imeonesha mtazamo wa wataalam mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada ya utafiti juu ya lugha ya kufundishia. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi, inafuatiwa na sehemu ya pili, ambayo ni mapitio kitaaluma ya kazi tangulizi, pengo la utafiti na sehemu ya mwisho ni hitimisho.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulika na mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika mchakato wa kufanya utafiti. Sehemu hii imeelezea eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, maadili ya utafiti, ukusanyaji na uchambuzi wa data, mkabala wa utafiti na mwisho ni muhtasari.

3.2 Usanifu na Mkabala wa Utafiti

Mtafiti amezipanga kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Mtafiti amekuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki na kutafsiri taarifa atakazozipata katika utafiti huu kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi.

Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki na kupangwa katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Data za aina moja zimewekwa pamoja ili kurahisisha usomaji wa maudhui yaliyokusudiwa.

Kuna mikabala mikuu miwili ya ukusanyaji na uwasilishaji wa data, mkabala wa kimaelezo na mkabala wa kitakwimu. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mikabala yote miwili. Mkabala wa kimaelezo, umetumika pasipo kufuata taratibu za kitakwimu kwa kutoa sababu zinazosababisha wanafunzi kuwa na ubobezi katika lugha na umilisi wao katika lugha ya kufundishia na kuzielezea data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti.

Kothari (1990), anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu. Anasema pia ni

kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoielezwa na walengwa wa utafiti. Mkabala wa kitakwimu/kiidadi, Mtafiti ametumia jedwali kuonesha data ambazo zimefupishwa kwa namna ambayo ni rahisi kuchambuliwa na kueleweka kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Data hizo ni yale majibu ya maswali ya utafiti jinsi wanafunzi walivyotoa majibu yao kususiana na malengo mahususi ya utafiti wetu.

Matinde (2014) anasema kuwa takwimu ni njia mahususi ya mawasiliano idhihirishayo kwa uwazi na uhakika chochote kile kinachohusika. Kwa hiyo data zilizokusanywa zimepangwa, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoielezwa na walengwa wa utafiti.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulihusu kupima ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili walichonacho wanafunzi wa darasa la VII dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia shule za msingi. Utafiti huu umefanyika katika Halmashauri ya wilaya ya Geita, Mkoani Geita. Mkoa wa Geita una Halmashauri sita ambazo ni Halmashauri ya mji Geita, Halmashauri ya wilaya ya Geita, Chato, Nyang'hwale, Mbogwe na Bukombe. Aidha Halmashauri ya wilaya ya Geita inazo kata 37. Miongoni mwa kata hizo ni kata Nyakamwaga ambapo ndipo mtafiti alifanya utafiti wake katika kata hii yenye idadi ya shule za msingi tano ambazo ni Nyakamwaga, Kashishi, Bufunda, Kasungamile na Buyagu.

Miongoni mwa sababu zilizopelekea mtafiti kuteua eneo hili la kufanyia utafiti ni pamoja na kuwa hakuna utafiti wowote uliofanyika katika eneo hili, aidha eneo lina

uwakilishi mzuri kwani ni eneo la kijijini mtafiti amepata picha halisi jinsi wanafunzi walivyo na umilisi wa lugha ya kufundishia tofauti na maeneo ya mijini ambapo muda mwingi wa mawasiliano hufanyika kwa lugha ya Kiswahili. Pia tafiti nyingi zimekuwa zikifanyika katika maeneo ya mijini na maeneo ya vijijini kusahaulika.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

3.4.1 Sampuli

Kwa mujibu wa Mligo (2012), sampuli ni kundi fulani la watu au vitu lililoko ndani ya mkusanyiko wa watu au vitu ambao mtafiti anaamini kwamba linazo habari zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti. Kuchagua sampuli ni kuchagua kundi dogo la watu au vitu katika mkusanyiko wenye makundi ya aina nyingi kwa malengo maalumu aliyonayo mtafiti kwa ajili ya utafiti wake. Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwatafiti wanafunzi wote wa darasa la saba katika wilaya ya Geita, mtafiti alifanya uteuzi wa sampuli ili kupata kundi dogo la watu watakaofanyiwa utafiti kuwakilisha kundi kubwa. Walengwa wa utafiti ni watu au vitu vyenye tabia, desturi na sifa zinazofanana. Kwa mujibu wa Koul (2009), walengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kwa hiyo, katika Utafiti huu kundi lengwa walikuwa wanafunzi wa darasa la saba wa shule za msingi katika kata ya Nyakamwaga yenye shule tano ambazo ni Bufunda, Nyakamwaga, Kashishi, Kasungamile na Buyagu wilayani Geita.

3.4.2 Usampulishaji

Ili kuweza kupata sampuli katika kazi ya utafiti ni lazima kufanya mchakato wa usampulishaji, ambao hutegemea mada husika na lengo la utafiti. Usampulishaji

kama alivyoeleza Adam (2008) ni mbinu, mchakato au kitendo cha kutafuta walengwa wa utafiti. Katika kufanya utafiti huu, walengwa walikuwa ni wanafunzi wa darasa la saba kwa shule za msingi katika kata ya Nyakamwaga wilayani Geita. Katika utafiti huu watafitiwa 100 waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu ikihusisha wanafunzi 20 kutoka kila shule.

3.5 Vyanzo vya Data

Utafiti umetumia aina mbili za data. Ambapo mtafiti ametumia data za msingi ambazo ni zile data alizopata kutoka kwa watafitiwa na data upili ni data ambazo alizipata kutoka maktabani kupitia vitabu na matini mbalimbali vya wataalamu wa lugha.

3.5.1 Data za Msingi

Kombo na Trombo (2006) wanasema kwamba data za msingi ni data zinazopatikana kutoka kwenye sampuli ya Utafiti au watafitiwa. Pia ni data zinazopatikana kutokana na maswali, mahojiano, kuonana ana kwa ana. Na data hizo ndio sababu ya kupatikana kwa data upili. Utafiti huu ulitumia data za msingi ambazo mtafiti alizipata kutoka kwa watafitiwa kupitia mahojiano ya ana kwa ana, zoezi la umilisi wa lugha na kupitia dodoso kutoka kwa watafitiwa juu ya ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili walichonacho wanafunzi wa darasa la VII.

3.5.2 Data Upili

Kwa mujibu wa Kothari (2004) data upili ni taarifa ambazo tayari zilishakusanywa na watu wengine. Katika ukusanyaji wa data, mtafiti alipata data hizi kutoka

maktabani kupitia vitabu, majarida, magazeti na makala mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti huu. Aidha, Kothari (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba, data upili zinaweza kuwa zimechapwa katika machapisho, vitabu, magazeti na matini.

Uso maji makini wa machapisho/nyaraka, katika ukusanyaji wa data za upili mtafiti alisoma kwa mzamo taarifa za matokeo ya wanafunzi ya mitihani ya mhula wa kwanza waliofanya wanafunzi na kuona ufaulu wao.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Kwa mujibu wa mada hii ya utafiti, mbinu tatu zimetumika kutupatia data; nazo ni zoezi la umilisi, hojaji, mahojiano na usomaji wa nyaraka/machapisho.

3.6.1 Zoezi la Umilisi

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu hii katika kukusanya na kutafuta data zilizohusiana na kiwango cha umilisi wa lugha walio nao wanafunzi. Katika mbinu hii mtafiti aliandaa maswali yaliyolenga kupata taarifa kuhusu umilisi walionao wanafunzi. Maswali haya yalilenga kutathimini uelewa wao katika utumizi wa lugha.

3.6.2 Mbinu ya Hojaji

Kwa mujibu wa Kothari (2012) mbinu ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali au dodoso yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Mbinu hii ni ya kutumia maswali yaliyoandikwa kwa lengo la kujibiwa na mtafitiwa. Aidha, Mligo (2012) anaendelea kudai kwamba, hojaji ni karatasi iliyoandikwa maswali ambayo hupewa mtafitiwa ili aandike majibu kulingana na maelezo ya wataalam hao, hojaji ni maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa lengo la kumhoji

mtafitiwa, na maswali haya yanafungamana na malengo ya utafiti husika, data hukusanywa kutokana na mtafitiwa kujibu maswali yaliyoorodheshwa katika karatasi.

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu hii katika kukusanya na kutafuta data zilizohusiana na kiwango cha ubobezi na umilisi wa lugha kwa wanafunzi kutokana na uwezo wao wa kiutendaji, kwa mfano, ujuzi wa mtafitiwa katika matumizi ya msamiati, usanifu wa lugha, kupima uwezo wa kutambua aina mbalimbali za maneno katika sentensi.

3.6.3 Mbinu ya Mahojiano /Usaili

Hii ni mbinu ambayo mtafiti anakusanya data akiwa ana kwa ana na mtafitiwa. Enon (1998) anafasili kuwa ni mbinu ya kuuliza maswali ya ana kwa ana, simu au barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu swali la utafiti lililoainishwa. Kothari (2004:97) anasema kuwa, njia hii hutumika kukusanya data na huwasilishwa kwa njia ya mdomo ana kwa ana baina ya mtafiti na mtafitiwa. Mtafiti ataweza kufafanua maswali ambayo hayaeleweki kwa mtafitiwa. Hali kadhalika mtafitiwa atapata nafasi ya kufafanua majibu au kumtaka Mtafiti kuliweka wazi swali ambalo halitaeleweka ipasavyo kwa Mtafitiwa.

Kwa hiyo mahojiano ni mbinu inayohusisha kujieleza kwa mdomo katika kuuliza na kujibu maswali. Lengo la kutumia mbinu ya mahojiano ni kulinganisha majibu yaliyopatikana kwa mbinu ya hojaji kupitia maswali dodoso ili kutafuta usahihi wa data zenyewe Aidha, uteuzi wa mbinu hii umezingatia lengo la kupata data ambazo

zisingeweza kupatikana kwa njia ya hojaji. Mbinu hii ilitumika katika kukusanya data zilizohusiana na malengo mahususi ya utafiti huu. Data hizo ni zile zinazohusiana na kwamba je wanafunzi wanao ujuzi au ufahamu wa lugha ya Kiswahili, sababu zinazochangia wanafunzi kuwa na ufahamu katika lugha ya Kiswahili na pia vigezo wanavyotumia kujiona kuwa wana ujuzi katika lugha ya Kiswahili.

3.6.4 Mbinu ya usomaji wa nyaraka/machapisho.

Katika kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alisoma kwa mzamo taarifa za matokeo ya wanafunzi ya mitihani ya mhula wa kwanza waliofanya wanafunzi na kuona ufaulu wao ili kufanya tathimini ya ufaulu wao kama unawiana na ubobezi waliouonyesha wakati wa kujibu maswali ya utafiti.

3.7 Maadili ya Utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu, ni lazima mtafitiwa aelezwe maadili ya utafiti ili aweze kutoa taarifa za ukweli na uhakika. Pons (1992), maadili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa na usiri yaani matafiti hatatoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Maelezo hayo yanafanana na yale ya Aeker (2002) kama alivyonyukuliwa na Adam (2008), waliotaja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya kuwa na usiri, yaani mtafiti kutotoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya

utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Kwa kuwa utafiti huu una madhumuni ya taaluma tu na si vinginevyo, maadili ya utafiti yalizingatiwa. Mtafiti alitambua haki zote hizi na kuzitekeleza kwa kuwaeleza watafitiwa maadili ya utafiti. Mtafiti pia aliwataka watafafitiwa kueleza kama wako tayari kushiriki katika utafiti.

3.8 Uchambuzi wa Data

Kothari (2008) anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Uchambuzi wa data utafanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kiidadi. Mbinu hizi zilistahili kwa sababu zilitoa maelezo na kutoa ufafanuzi kuhusu ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili walichonacho wanafunzi wa darasa la VII. Data zilihakikiwa na kupitiwa kwa makini kwa kupangwa katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Data za aina moja zimewekwa pamoja ili kurahisisha usomaji wa maudhui yaliyokusudiwa.

3.9 Muhutասari

Sura hii imechambua mbinu za utafiti. Eneo la utafiti limetajwa kuwa ni katika kata ya Nyakamwaga yenye shule za msingi tano, sampuli na usampulishaji, walengwa wa utafiti wameainishwa kuwa ni wanafunzi wa darasa la saba shule za msingi, njia ya mahojiano, hojaji na zoezi la umilisi wa lugha zimeelezwa kuwa zilitumika katika

kukusanya data za utafiti. Maadili ya utafiti yameelezwa. Uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya yameelezwa kwa ufupi pia.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha data zilizopatikana uwandani. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981). Misingi hiyo ni uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo.

Uwasilishaji wa data umefanyika kinaelezo na kitakwimu, maelezo yalitolewa kwa ufupi huku yakiambatanishwa na majedwali yenye takwimu. Uchambuzi wa data ulilenga kujibu maswali ya utafiti huu katika kukamilisha malengo ya utafiti. Uchambuzi wa data umehusishwa na malengo mahsusi ya utafiti huu na kwa kujibu maswali ya utafiti.

Katika utafiti huu, data zilizopatikana zilichambuliwa na kuhakikiwa kwa kina. Data zilihakikiwa na kupitiwa kwa makini kwa kupangwa katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Data za aina moja ziliwekwa pamoja ili kurahisisha usomaji wa maudhui yaliyokusudiwa. Uchambuzi wa data umehusiana na malengo mahsusi ya utafiti huu na kuona ukweli ambao umepatikana kwa njia ya hojaji, mahojiano, zoezi la umilisi wa lugha na mbinu ya usomaji wa nyaraka.

Baada ya kukusanya taarifa na kuzipanga pamoja, uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kuangalia takwimu ya majibu ya wanafunzi juu ya ubobezi wao katika lugha ya

Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa shule za msingi na Kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia shule za msingi. Majibu ya aina moja yamewekwa pamoja na kufanyiwa asilimia. Matokeo ya taarifa yametolewa maelezo pamoja na kuchanganuliwa kwa njia ya majedwali na maelezo ili kuweka wazi matokeo yake.

Utafiti huu umehusisha wanafunzi wa darasa la saba (VII) katika kata ya Nyakamwaga yenye shule za serikali tano (5), ambazo ni Nyakamwaga, Kashishi, Bufunda, Kasungamile na Buyagu. Jumla ya wanafunzi waliotafitiwa walikuwa 100, wanafunzi 20 toka kila shule. Shule za msingi hizo ambazo zilifanyiwa utafiti, pamoja na wanafunzi 20 waliofanyiwa utafiti shule hizo zina wanafunzi wa darasa la saba kama ifuatavyo:

Jedwali 4.1 : Idadi ya Wanafunzi Wa Darasa la Saba Katika Shule za Kata ya Nyakamwaga

Sn	Shule	Idadi ya wanafunzi	Waliofanyiwa utafiti	Asilimia
1	Buyagu	56	20	35.7
2	Nyakamwaga	37	20	54.0
3	Kasungamile	32	20	62.5
4	Bufunda	49	20	40.8
5	Kashishi	31	20	64.5
	Jumla	205	100	49

Chanzo: Taarifa za Tasinifu (2019)

Kama jedwali linavyoonesha hapo. Katika shule hizo wapo jumla ya wanafunzi 205 kati yao wanafunzi 100 sawa na asilimia 49 walifanyiwa utafiti huu.

4.2 Ubobezi wa Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi

Madhumuni mahususi ya kwanza katika utafiti huu yalilenga kupima ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa shule za msingi. Sehemu hii inawasilisha matokeo na kujadili upimaji uliofanyika kwa wanafunzi juu ya ubobezi wao katika lugha ya kufundishia.

4.2.1 Tathmini binafsi ya Ujuzi au Ufahamu Katika Lugha ya Kiswahili

Mtafiti alitumia maswali ya usaili ambayo yalilenga watafitiwa kujifanyia tathmini kama wanaamini wanao ujuzi wa lugha ya kiswahili. Mtafiti aliwataka watafitiwa kusema kama wana ufahamu au ujuzi wa lugha ya Kiswahili au laa. Majibu ya wanafunzi yanaonesha kuwa wote walijibu kuwa wana ujuzi wa lugha ya Kiswahili.

Jedwali 4.2: Matokeo ya Watafitiwa Kuhusu Ufahamu au Ujuzi wa Lugha ya Kiswahili

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Ndiyo	%	Hapana	%
Bufunda	20	100	20	100	0	0
Buyagu	20	100	20	100	0	0
Kashishi	20	100	20	100	0	0
Kasungamile	20	100	20	100	0	0
Nyakamwaga	20	100	20	100	0	0
Jumla	100	100	100	100	0	0

Chanzo: Taarifa za Tasinifu (2019)

Jedwali 4.2 linaonesha watafitiwa wote wanaujuzi na ufahamu wa lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanadhihirisha kwamba watafitiwa wanaamini kuwa na ujuzi na ufahamu wa lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanalandana na maoni ya Msanjila na wenzake (2011) wanaposema kwamba, matumizi ya lugha sahihi katika

kufundishia masomo katika mfumo wa elimu ni zaidi ya kuwasaidia wanaojifunza kwa sababu huendeleza pia vipaji vyao na kubwa zaidi lugha hiyo huendelezwa ili kukabili mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mtafiti pia aliwataka watafiwa kubaini ni vigezo gani vinavyowafanya wajione kuwa wana ujuzi/ufahamu katika lugha ya Kiswahili. Watafitiwa walisema kuwa vigezo vinavyowafanya wajione kuwa wana ujuzi na ufahamu katika lugha ya Kiswahili ni kutokana na kuwa wana uwezo wa kuzungumza lugha ya kiswahili, kusikiliza na kuelewa sentensi zinazoongelewa na watu wengine kwa kutumia lugha ya Kiswahili, kusoma maandiko na kuandika vizuri kwa kutumia lugha ya Kiswahili, Aidha wana uwezo wa kutambua maneno mbalimbali ya Kiswahili na pia kuweza kung'amua kuwa neno fulani sii neno la lugha ya Kiswahili. Majibu haya yanatupa mwelekeo na kuashiria kuwa watafitiwa wana ujuzi au ufahamu wa kutosha katika lugha ya Kiswahili.

(1)

MAHOJIANO KWA AJILI YA WANAFUNZI

Taarifa za awali za wahojiwa

Maswali kwa ajili ya wanafunzi

Taarifa za awali

Jinsi me () ke ()

Darasa VII

Umri (miaka) 12

Jina la Shule BUPHUNDA

Kata DYAKAMWAGA

Wilaya GETTA

Mkoa GETTA

Tarehe 4.6.2019

Jibu maswali yafuatayo kwa usahihi.

1. Je unao ujuzi au ufahamu wa kutosha wa lugha ya Kiswahili?

NDIO NIKAO

2. Kwa vigezo gani unajiona unao/huna huo ujuzi/ufahamu ?

KWA SABABU NAWAZA KUWASILIANA NA WATU WA NIPWAELE
WA VIZURI.

3. Taja sababu zinazochangia wewe kama mwanafunzi kuwa na ufahamu katika lugha ya kiswahili

KISWAHIKI KINAFUANKA MUDA MWINAZI WA MPONGEZI

Mchoro 4.1 : Maswali na Majibu kwa ajili ya Wanafunzi

Majibu ya mahojiano mtafiti alikuwa anatomia karatasi kuweka nukuu ya yale yaliyokuwa yanasemwa na watafitiwa lakini baadhi ya watafitiwa kwa maoni yao walipenda pia wanapo jibu katika maongezi waweke nukuu kwenye karatasi ili waweze kujibu kwa uhakika zaidi juu ya kile walichoulizwa na mtafiti. Kwa hali hiyo mtafiti aliwapa uhuru wa kile walichokitaka ili mradi waweze kujibu maswali

ya utafiti ipasavyo. Miongoni mwa majibu ya mahojiano ya wanafunzi yalikuwa kama yalivyoambatanishwa hapo juu ambapo swali la kwanza ndilo linalohusika.

4.2.2 Ufahamu wa Wanafunzi katika Kutambua na Kubaini Aina za Maneno

Mtafiti alitumia hojaji kwa njia ya maswali dodoso kuwauliza wanafunzi watambue na kubaini aina za maneno katika sentensi mbalimbali. Maswali hayo yalilenga kupima uwezo wa mtafitiwa wa kutambua na kubaini aina za maneno katika sentensi mbalimbali. Matokeo yalionesha kuwa watafitiwa 87 kati ya 100 sawa na asilimia 87 waliweza kutambua na kubaini aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili na wanafunzi 13 sawa na asilimia 13 hawakuweza kubaini aina za maneno katika sentensi mbalimbali. Matokeo ya watafitiwa kuhusu kubaini na kutambua aina za maneno katika sentensi mbalimbali ni kama yalivyowasilishwa kwenye jedwali 4.3 lifuatalo:

Jedwali 4.3 : Matokeo Kubaini na Kutambua Aina aa Maneno

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Walioweza	%	wasioweza	%
Bufunda	20	100	17	85	3	15
Buyagu	20	100	19	95	1	5
Kashishi	20	100	16	80	4	20
Kasungamile	20	100	17	85	3	15
Nyakamwaga	20	100	18	90	2	10
Jumla	100	100	87	87	13	13

Chanzo: taarifa za tasinifu (2019)

Jedwali 4.3 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa, sawa na asilimia 87, waliweza kubaini na kutambua aina za maneno katika sentensi na asilimia 13 ya watafitiwa hawakuweza kubaini aina za maneno. Watafitiwa walipewa sentensi ili waweze kubaini neno ‘ mkali ’ ni aina gani ya neno katika sentensi hii : ‘Mnyama

mkali amekamatwa leo'. Katika kujibu swali hili watafitiwa 13 waliokosa swali hili, majibu yao yalikuwa : *neni hili mkali ni kiwakilishi*, walishindwa kung'amua kuwa kiwakilishi huwepo katika sentensi badala ya nomino. Sasa katika sentensi hiyo nomino tayari ilikuwepo ambayo ni 'mnyama', kwa hali hiyo neno hilo lilikuwa ni kivumishi

ZOEZI KWA AJILI YA WANAFUNZI LA KUPIMA UFAHAMU WA LUGHA

Taarifa za awali za wahojiwa

Jinsi me () ke ()

Darasa VII

Umri (miaka) 12

Jina la Shule BUFUNDA

Kata NYAKANWAGA

Wilaya GETTA

Mkoa GETTA

Tarehe 4/6/2019

Chagua jibu sahihi kwa kuweka herufi ya jibu katika kisanduku ulichopewa.

1. "Yeye amefaulu mitihani yake vizuri". Katika sentensi hii neno lipi limetumika kama kitenzi?

a) yeye
b) amefaulu
c) mitihani
d) yake

(B)

2. "Mnyama mkali amekamatwa leo." Katika sentensi hii neno "mkali" limetumika kama aina gani ya neno ?

a) kielezi
b) kiwakilishi
c) kivumishi
d) kitenzi

(C)

3. "Kitabu changu ni cheusi, chako ni cheupe." Neno "chako" ni aina gani ya neno ?

2

- a) kivumishi
- b) kiwakilishi
- c) kielezi
- d) kihusishi

(B)

4. "Siku ile ya maandamano kulikuwa na wa pikipiki". Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo ?

- a) msururu
- b) msurulu
- c) msululu
- d) musururu

(A)

5. Tulihudhuria kwenye ya kumuaga dada yetu.

- a) tahadhari
- b) taharuki
- c) tafrija
- d) frija

(C)

6. Kinyume cha kitenzi "paa" ni kipi?

- a) Toweka
- b) Elea
- c) Shuka
- d) Tua

(D)

7. "Hapa alipoishi chifu wa wanyaturu"

Data hizo hapo juu zinadhihirisha kwamba wanafunzi walio wengi sawa na asilimia 87 waliweza kubaini aina za maneno hivyo wana ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa shule za msingi. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni kama ulivyo katika Mchoro 4.2 ambapo swali la 1 la 2 na la 3 ndio yaliyohusika juu ya kubaini na kutambua aina mbalimbali za maneno katika sentensi.

4.2.3 Uwezo wa Wanafunzi katika Matumizi ya Msamiati na Usanifu wa Lugha

Mtafiti alitumia hojaji kupima ujuzi wa watafitiwa katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha. Matokeo ya watafitiwa 89 kati ya 100 sawa na asilimia 89 waliweza kubaini matumizi ya msamiati sahihi na usanifu wa lugha katika sentensi na wanafunzi 11 sawa na asilimia 11 hawakuweza kubaini matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha katika sentensi mbalimbali. Matokeo ya watafitiwa kuhusu kubaini matumizi ya msamiati sahihi na usanifu wa lugha ni kama yalivyowasilishwa kwenye jedwali 4.4.

Jedwali 4.4: Matokeo ya Matumizi ya Msamiati Sahihi na Usanifu wa Lugha

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Waliopata yote	%	wasiokosa	%
Bufunda	20	100	19	95	1	5
Buyagu	20	100	18	90	2	10
Kashishi	20	100	18	90	2	10
Kasungamile	20	100	17	85	3	15
Nyakamwaga	20	100	17	85	3	10
Jumla	100	100	89	89	11	11

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.4 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa sawa na asilimia 89 waliweza kubaini matumizi ya msamiati sahihi na usanifu wa lugha na asilimia 11 ya

watafitiwa hawakuweza kubaini aina za maneno. Watafitiwa 11 waliokosa swali hili ambalo lilikuwa ni kubaini msamiati sahihi ili kukamilisha sentensi hii “Siku ile ya maandamano kulikuwa na wa pikipiki” wengi wao walichagua jibu kuwa ni ‘msululu’ badala jibu sahihi ambalo lilikuwa ni ‘msururu’. Hii ni kutokana na athari ya lugha mama, kama anavyosema Rocha (2011) kuwa wabantu wengi wameathiriwa na lugha mama. Wengi wa watafitiwa katika eneo lililofanyiwa utafiti ni wa kabila la wasukuma ambao hutumia fonimu ‘l’ badala ya ‘r’ ndio maana wachache wao wakashindwa kung’amua neno sahihi ambalo ni msururu.

2

a) kivumishi
b) kiwakilishi
c) kielezi
d) kihusishi

4. “Siku ile ya maandamano kulikuwa na wa pikipiki”. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo ?

a) msururu
b) msurulu
c) msululu
d) musururu

5. Tulihudhuria kwenye ya kumuaga dada yetu.

a) tahadhari
b) taharuki
c) tafrija
d) frija

6. Kinyume cha kitenzi “paa” ni kipi?

a) Toweka
b) Elea
c) Shuka
d) Tua

7. “Hapa alipoishi chifu wa wanyaturu”

Mchoro 4.3: Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Nne

Yakichunguzwa matokeo ya watafitiwa waliowengi yanaakisi kwa kiasi kikubwa kuwa wengi wa watafitiwa wana ufahamu mzuri katika matumizi sahihi ya msamiati na usanifu wa lugha na hivyo wana ufahamu katika lugha ya Kiswahili kama lugha

ya kufundishia. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni kama ulivyo katika Mchoro 4.3 ambapo swali la 4 ndio lililohusika juu ya matumizi sahihi ya msamiati.

4.2.4 Ufahamu katika Muundo wa Sentensi

Kwa kutumia hojaji mtafitiwa alitumia maswali ya kupima ujuzi walionao watafitiwa katika sarufi ya lugha kuhusu muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi. Matokeo ya watafitiwa 89 kati ya 100 sawa na asilimia 89 waliweza kubaini matumizi ya neno sahihi ambalo linapaswa kuwekwa ili sentensi iwe sahihi kwa kuzingatia muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi na wanafunzi 11 sawa na asilimia 11 hawakuweza kubaini muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi katika sentensi mbalimbali. Matokeo ya watafitiwa kuhusu kubaini muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi ni kama yalivyowasilishwa kwenye jedwali 4.5.

Jedwali 4.5 : Ufahamu wa Matumizi ya Muundo wa Sentensi Katika Upatanisho Wa Kisarufi

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Waliopata yote	%	Wasiokosa	%
Bufunda	20	100	18	90	2	10
Buyagu	20	100	19	95	1	05
Kashishi	20	100	18	90	2	10
Kasungamile	20	100	17	85	3	15
Nyakamwaga	20	100	17	85	3	15
Jumla	100	100	89	89	11	11

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.5 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa sawa na asilimia 89 waliweza kubaini muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi na

asilimia 11 ya watafitiwa hawakuweza kubaini aina za maneno katika sentensi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Wengi wa wanafunzi waliokosa swali hili walichagua jibu ambalo halikuwa sahihi katika kukamilisha sentensi: “Hapa alipoishi chifu wa wanyaturu” kwa kuchagua jibu la ‘ndio’ badala ya jibu sahihi ambalo lilikuwa ‘ndipo’. Wanafunzi hao walishindwa kugundua kuwa upatanisho uliopo ni ule wa kiwakilishi ‘hapa’ na kielezi kinahitaji ukamilifu wake wa neno lenye upatanisho wa kisarufi ili ilete maana iliyosahihi.

2

a) kivumishi
b) kiwakilishi
c) kielezi
d) kihusishi

4. “Siku ile ya maandamano kulikuwa na wa pikipiki”. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo ?

a) msururu
b) msurulu
c) msululu
d) musururu

5. Tulihudhuria kwenye ya kumuaga dada yetu.

a) tahadhari
b) taharuki
c) tafrija
d) frija

6. Kinyume cha kitenzi “paa” ni kipi?

a) Toweka
b) Elea
c) Shuka
d) Tua

7. “Hapa alipoishi chifu wa wanyaturu”

3

a) ndiko
b) ndimo
c) ndio
d) ndipo

8. Yeye ni kijana mdogo. Neno "yeye" lipo katika nafsi gani ?

a) Ya kwanza umoja
b) Ya tatu umoja
c) Ya pili umoja
d) Ya tatu wingi

9. Atakapomnyonyoa yule bata kwenye moto.

a) Atambanika
b) Anambanika
c) Amembanika
d) Alimbanika

10. "Walikotoka kuna mvua." Sentensi hiyo ipo katika wakati gani ?

a) Wakati uliopo
b) Wakati uliopita
c) Wakati ujao
d) Wakati wa sasa

Asante kwa ushirikiano wako

Mchoro 4.4 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Saba

Kutokana na majibu ya watafitiwa ya swali la dodoso yalionesha kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi waliweza kujibu swali lililohusiana na muundo wa sentensi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Hiki ni kiashiria tosha kuwa watafitiwa wetu wana ufahamu mzuri wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na wana ujuzi wa kutosha katika lugha ya Kiswahili. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni kama ulivyo hapa chini ambapo swali la 7 ndilo lililohusika katika sarufi ya lugha kuhusu muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi.

4.2.5 Utambuizi wa Matumizi ya Nafsi katika Tungo

Mtafiti alitumia hojaji kuwaomba wanafunzi kujibu swali ambalo lilihitaji watambue matumizi ya nafsi katika tungo. Swali hili lililenga kupima uwezo wa kutambua matumizi ya nafsi katika tungo. Matokeo ni kwamba watafitiwa 93 kati ya 100 sawa

na asilimia 93 waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kutambua matumizi ya nafsi katika tungo za lugha ya Kiswahili na wanafunzi 7 tu sawa na asilimia 7 hawakuweza kujibu swali kwa usahihi na kushindwa kutambua matumizi ya nafsi katika tungo za lugha ya Kiswahili. Matokeo ya watafitiwa kuhusu kutambua matumizi ya nafsi katika tungo za lugha ya Kiswahili ni kama yalivyowasilishwa kwenye Jedwali 4.6.

Jedwali 4.6 : Matokeo Kuhusu Kutambua Matumizi ya Nafsi katika Tungo

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Walioweza	%	wasioweza	%
Bufunda	20	100	20	100	0	0
Buyagu	20	100	18	90	2	10
Kashishi	20	100	18	90	2	10
Kasungamile	20	100	18	90	2	10
Nyakamwaga	20	100	19	95	1	5
Jumla	100	100	93	93	7	7

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.6 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa sawa na asilimia 93 waliweza kutambua matumizi ya nafsi katika tungo za lugha ya Kiswahili na asilimia 7 ya watafitiwa hawakuweza kutambua matumizi sahihi ya nafsi katika tungo za lugha ya Kiswahili. Katika sentensi walilopewa wanafunzi: ‘Yeye ni kijana mdogo’ walitakiwa kubaini neno “yeye” lipo katika nafsi gani ?. Majibu ya watahiniwa waliokosa swali hili walisema neno hilo liko katika nafsi ya pili badala ya jibu sahihi ambalo lilikuwa ni nafsi ya tatu.

Data hizo hapo juu zinadhihirisha kwamba wengi wa wanafunzi kwa ujumla wao waliofikia asilimia 93, wana ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa shule za msingi katika nyanja ya Isimu. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni

kama ulivyo hapa chini ambapo swali la 8 ndilo lililohusika katika kupima uwezo wa kutambua matumizi ya nafsi katika tungo.

3

a) ndiko
b) ndimo
c) ndio
d) ndipo

8. Yeye ni kijana mdogo. Neno "yeye" lipo katika nafsi gani ?

a) Ya kwanza umoja
b) Ya tatu umoja
c) Ya pili umoja
d) Ya tatu wingi

9. Atakapomnyonyoa yule bata kwenye moto.

a) Atambanika
b) Anambanika
c) Amembanika
d) Alimbanika

10. "Walikotoka kuna mvua." Sentensi hiyo ipo katika wakati gani ?

a) Wakati uliopo
b) Wakati uliopita
c) Wakati ujao
d) Wakati wa sasa

Asante kwa ushirikiano wako

Mchoro 4.5: Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa

4.2.6 Ufahamu wa Matumizi ya Njeo

Kwa kutumia maswali ya hojaji, mtafiti alipima uwezo wa watafitiwa katika matumizi ya njeo (nyakati).

4.2.6.1 Ufahamu wa Matumizi ya Njeo Katika Sentensi

Kwa kutumia maswali ya hojaji, mtafiti alipima uwezo wa watafitiwa katika matumizi ya njeo, Mtafiti aliwataka watafitiwa kubaini sentensi waliopewa iko katika wakati gani. Matokeo ya watafitiwa yameonesha kuwa watafitiwa 95 kati ya 100 sawa na asilimia 95 walikuwa na uwezo katika kutumia maneno yanayoonesha

nyakati mbalimbali katika lugha ya kiswahili na watafitiwa 5 sawa na asilimia 5 walishindwa swali lililohusu matumizi ya njeo katika lugha ya kufundishia ya kiswahili. Matokeo ya watafitiwa kuhusu uwezo wao katika matumizi ya njeo (nyakati) ni kama yalivyowasilishwa kwenye jedwali 4.7.

Jedwali 4.7: Ufahamu wa Matumizi ya Njeo

Shule	Idadi watafitiwa	ya	%	Waliopata	%	wasiokosa	%
Bufunda	20		100	19	95	1	5
Buyagu	20		100	20	100	0	0
Kashishi	20		100	18	90	2	10
Kasungamile	20		100	18	90	2	10
Nyakamwaga	20		100	20	100	0	0
Jumla	100		100	95	95	5	5

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.7 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa, sawa na asilimia 95, walionesha kujua matumizi ya maneno katika nyakati mbalimbali na watafitiwa 5 sawa na asilimia 5 ya watafitiwa hawakuweza kubaini maneno katika nyakati. Katika sentensi waliopewa wanafunzi : “Walikotoka kuna mvua.” walipotakiwa kubainisha sentensi hiyo ipo katika wakati gani, walichagua jibu kuwa ipo katika wakati uliopita jibu ambalo halikuwa sahihi. Sentensi hii ina tungo tegemezi na tungo kuu ambapo tungo tegemezi ni ‘walikotoka’ na tungo kuu ni ‘kuna mvua’ kwa viwango vyao wanafunzi wa shule za msingi katika kuzitofautisha njeo katika nyakati mbalimbali, zimebainishwa katika namna tatu. Yaani, kuna njeo ya wakati tulionao yenye kuwakilishwa na mofimu ‘-na-’, njeo ya wakati ujao inayowakilishwa kwa ‘-ta-’, na njeo ya wakati uliopita ambayo huwakilishwa kwa ‘-me-’ iwapo wakati uliopita ni muda mfupi, na kwa ‘-li-’ iwapo umepita muda mrefu.

3

- a) ndiko
- b) ndimo
- c) ndio
- d) ndipo

D

8. Yeye ni kijana mdogo. Neno "yeye" lipo katika nafsi gani ?

- a) Ya kwanza umoja
- b) Ya tatu umoja
- c) Ya pili umoja
- d) Ya tatu wingi

B

9. Atakapomnyonya yule bata kwenye moto.

- a) Atambanika
- b) Anambanika
- c) Amembanika
- d) Alimbanika

A

10. "Walikotoka kuna mvua." Sentensi hiyo ipo katika wakati gani ?

- a) Wakati uliopo
- b) Wakati uliopita
- c) Wakati ujao
- d) Wakati wa sasa

B

Asante kwa ushirikiano wako

Mchoro 4.6: Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Tisa

Huenda neno 'walikotoka' ambalo lina mofimu -li- ndiyo lililowavutia watahiniwa hao kutoa jibu hilo wakidhani kuwa ndilo lililobeba sentensi nzima badala yake walipaswa wazingatie tungo kuu inayosema kuwa 'kuna mvua' ambayo ndio iko katika wakati uliopo. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa watafitiwa asilimia kubwa wana uwezo na umilisi katika lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni kama ulivyo hapa chini ambapo swali la 9 na la 10 ndio yaliyohusika katika matumizi ya njeo.

4.2.6.2 Uwezo Wa Wanafunzi Kutunga Sentensi Kwa Kutumia Mofimu za Njeo

Kwa kutumia maswali ya hojaji, mtafiti alipima uwezo wa watafitiwa katika kutunga sentensi kwa kutumia mofimu za njeo. Mtafiti aliwataka watafitiwa kutunga sentensi kwa kutumia mofimu za njeo walizopewa wakitumia mofimu –li- kutunga sentensi iliyo katika wakati uliopita. Mofimu –na- kutunga sentensi ambayo iko katika wakati uliopo na mofimu –ta- kutunga sentensi ambayo ipo katika wakati ujao. Matokeo ya watafitiwa yameonesha kuwa watafitiwa wote 100 sawa na asilimia 100 waliweza kutunga sentensi kwa kutumia mofimu hizo za wakati. Matokeo ya watafitiwa kuhusu uwezo wao katika kutunga sentensi kwa kutumia mofimu za njeo ni kama yalivyowasilishwa kwenye jedwali 4.8 lifuatalo hapa chini:

Jedwali 4.8: Ufahamu wa Matumizi ya Njeo

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Waliopata	%	wasiokosa	%
Bufunda	20	100	20	100	0	0
Buyagu	20	100	20	100	0	0
Kashishi	20	100	20	100	0	0
Kasungamile	20	100	20	100	0	0
Nyakamwaga	20	100	20	100	0	0
Jumla	100	100	100	100	0	0

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.8 linaonesha kwamba watafitiwa wote waliweza kutunga sentensi Matokeo haya yanadhihirisha kuwa watafitiwa wana uwezo mkubwa na umilisi katika lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni kama ulivyo hapa chini ambapo swali la 4 ndilo lililohusika katika kuwapima watafitiwa uwezo wao katika kutunga sentensi kwa kutumia mofimu za njeo.

②

Maongozi yetu w walim w wanafunzi tuitam. Kweli

4. Tunga sentensi moja moja kwa kila nyakati kwa kuzingatia mofimu ya waakati uliopewa

i) wakati uliopita mofimu -li-
Mwalim alitufundisha namna ya kufua nguo.

ii) wakati uliopo kwa kutumia mofimu -na-
Ng'ombe anakunyua maji

iii) Wakati ujao kwa kutumia mofimu -ta-
Wanafunzi taka mwanzo watawahi jiwa ya leo

Asante kwa ushirikiano wako.

Mchoro 4.7 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la Nne

4.2.7 Uelewa wa Watafitiwa katika Utumizi wa Lugha

Mtafiti alitumia zoezi la umilisi kwa kuwapatia watafitiwa maswali ambayo yalilenga kujua uelewa wao katika utumizi wa lugha, Maswali yalikuwa ni sentensi ambazo baadhi zilikuwa sahihi na zingine hazikuwa sahihi, mtafiti aliwataka watafitiwa kubaini sentensi ambazo wanadhani ziko sahihi kwa kuweka alama ya vema mbele ya kisansuku walichopea na kuweka alama ya kosa mbele ya sentensi ambayo walidhani kuwa haiko sahihi. Maswali haya yalilenga kujua uelewa wao katika utumizi wa lugha kwa kutambua sentensi sahihi na zilizo katika muundo sahihi wa lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya watafitiwa yameonesha kuwa watafitiwa wote 100 sawa na asilimia 100 waliweza kubaini sentensi ambazo ziko sahihi na ambazo haziko sahihi kimuundo katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya watafitiwa kuhusu uelewa wao katika utumizi wa lugha ni kama yalivyowasilishwa kwenye jedwali 4.9 lifuatalo hapa chini:

Jedwali 4.9 : Matokeo ya Watafitiwa Kuhusu Uelewa wa Watafitiwa Katika Utumizi Wa Lugha

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Waliopata	%	waliokosa	%
Bufunda	20	100	20	100	0	0
Buyagu	20	100	20	100	0	0
Kashishi	20	100	20	100	0	0
Kasungamile	20	100	20	100	0	0
Nyakamwaga	20	100	20	100	0	0
Jumla	100	100	100	100	0	0

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.9 linaonesha kwamba watafitiwa wote sawa na asilimia 100 wana uelewa katika utumizi wa lugha kwa kutambua sentensi sahihi na zilizo katika muundo sahihi wa lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa watafitiwa wanaujuzi na ufahamu mzuri wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa kuwa waliweza kubaini sentensi zilizosahihi na ambazo sio sahihi za lugha ya Kiswahili.

Matokeo haya yanakubalina na Peterson (2006) ambaye anayesema kuwa, wanafunzi wana mawazo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hawa wanaelewa zaidi wanapofundishwa katika lugha ya Kiswahili ambayo wanaitumia hata nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku, wanapofundishwa kwa lugha hiyo wanapata maarifa kamili kuliko wanapofundishwa kwa lugha ziningine kama vile Kiingereza. Ushahidi juu ya majibu ya watafitiwa ni kama ulivyo hapa chini ambapo swali la 4 ndilo lililohusika katika maswali ambayo yalilenga kujua uelewa wao katika utumizi wa lugha.

(1)

ZOEZI LA UMILISI WA LUGHA

Taarifa za awali za wahojiwa

Jinsi me () ke (✓)
 Darasa VII
 Umri (miaka) 12
 Jina la Shule BUFUNDA
 Kata NYAKALWAGA
 Wilaya GELTA
 Mkoa GELTA
 Tarehe 4.6.2019

Weka alama ya vema kwenye jibu ambalo ni sahihi:

1. Je, unapendelea kutumia lugha gani zaidi katika mijadala/majadiliano ya mada za masomo unayofundisha hapa shuleni ?

✓ Kiswahili (✓), kiingereza (), kisukuma (), nyingine ()

Unapokuwa unafanya mawasiliano na walimu wako unatumia lugha gani ?

✓ Kiswahili (✓), kiingereza (), kisukuma (), nyingine ()

Unapokuwa katika shughuli za nje ya darasa mfano katika michezo au shughuliza uzalishaji shuleni unatumia lugha gani?

✓ Kiswahili (✓), kiingereza (), kisukuma (), nyingine ()

Weka alama ya vema mbele ya sentensi ambayo unadhani kuwa iko sahihi na alama ya kosa mbele ya sentensi ambayo unadhani haiku sahihi.

Mchoro 4 :8 ushahidi juu lugha wanayotumia wanafunzi.

2 ✓

Nitakuja kwako ijumaa ijayo (✓)

Masanja aliondoka kesho (✗)

Ng'ombe wangu wamepotea (✓)

Viti hizi zimeharibika (✗)

Mwalimu aliyekuja jana ameondoka kesho asubuhi (✗)

Nimekuja hapa tangia asubuhi (✗)

Nimekuja hapa tangu asubuhi (✓)

Dada anamwandikiaga barua baba (✗)

Mapanya hawa wanakula unga wetu (✗)

Mariam na Pendo anaondoka keshokutwa (✗)

Asante kwa ushirikiano wako

Mchoro 4.9 : Ushahidi juu ya Majibu ya Watafitiwa Swali la 4

Katika mchoro 4.8 wanafunzi walitakiwa kusoma maelezo na kuchagua katika orodha ni lugha ipi wanayotumia wakiwa katika mazingira mbalimbali. wanafunzi wote walisema wanatumia lugha ya kiswahili wakiwa katika mazingira mbalimbali na pia. Katika mchoro 4.9 wanafunzi walitakiwa kuzisoma sentensi ambazo walipewa, baadhi ya sentensi zilikuwa sahihi na zingine hazikuwa sahihi, wanafunzi walitakiwa kuweka alama ya vema mbele ya sentensi ambayo waludhani kuwa iko sahihi na kuweka alama ya kosa mbele ya sentensi ambayo walidhani kuwa haiko sahihi.

4.2.8 Sababu Zinazochangia Watafitiwa Kuwa Na Ufahamu Katika Lugha ya Kiswahili

Mtafiti alitumia maswali ya usaili yaliyolenga kujua sababu zinazochangia watafitiwa kuwa na ufahamu katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alifanya mahojiano na watafitiwa 86 kati ya 100 waliotarajiwa kufanyia utafiti sawa na asilimia 86, wanafunzi 14 sawa na asilimia 14 hawakufanyiwa utafiti kwa sababu hawakuwepo shuleni wakati mtafiti alipokuwa anafanya usaili.

Jedwali 4.10: Watafitiwa Waliokuwepo Wakati wa Usaili

Shule	Idadi ya watafitiwa	%	Waliokuwepo	%	Wasiokuwepo	%
Bufunda	20	100	16	80	4	20
Buyagu	20	100	18	90	2	10
Kashishi	20	100	17	85	3	15
Kasungamile	20	100	18	90	2	10
Nyakamwaga	20	100	17	85	3	15
Jumla	100	100	86	86	14	14

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.10 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa sawa na asilimia 86 walikuwepo wakati wa kujibu maswali ya usaili katika kutoa sababu zinazochangia wao kuifahamu lugha ya kiswahili.

Watafitiwa waliweza kutoa sababu mbalimbali zinazochangia wao kuwa na ufahamu katika lugha ya kiswahili. Sababu hizo ni pamoja na kuwa Kiswahili kinatumika muda mwingi wa maongezi ya watafitiwa wanapokuwa shuleni baina yao na wanafunzi wengine na baina yao na walimu wao wakati wa ujifunzaji na ufundishaji aidha mawasiliano yote rasmi yanayofanyika shuleni, lugha ya Kiswahili ndio lugha

itumikayo katika kutolea matangazo na maelekezo shuleni, Aidha mawasiliano baina ya watafitiwa na walimu wao hufanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili na Ufundishaji wa masomo ya darasani lugha ya Kiswahili inatumika, hoja hii inalandana na hoja ya Rubagumya (2003) anayedai kwamba ufundishaji unaotumia lugha inayofahamika baina ya walimu na wanafunzi huleta ufanisi wa kutosha kwa sababu wanafunzi watajua jinsi ya kutumia maarifa ya kidhanifu katika taarifa mpya.

Rubagumya (keshatajwa) anaenelea kudai kwamba, lugha inapokuwa ni ile iliyozoeleka kwa wanafunzi na ambayo walimu wanaimudu vyema huuleta uelewa mzuri wa dhana ya somo linalofundishwa. Pia vitabu vingi vya hadithi ambavyo vinatumia na kusomwa na wanafunzi vimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya kwanza au ya pili kwa watanzania walio wengi. Kiswahili ni lugha ya kwanza kwa baadhi ya watanzania na ya pili kwa wengine, ambayo mtoto hukua nayo. Lakini pia, Kiswahili ndiyo lugha ya kufundishia elimu ya awali na ya msingi.

Wengi wa wanafunzi wanapokuwa nyumbani na wazazi wao ama walezi wao au katika jamii wanayoishi lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumika; Hii ni kutokana na mchanganyiko wa jamii wanapoishi wanafunzi kwani yapo makabila mbalimbali ambayo huishi pamoja na ili mawasiliano yafanyike kiamilifu na kwa maelewano, Kiswahili ndiyo lugha pekee inayowaunganisha wanajamii wote. Katika kata ya Nyakamwaga, baadhi ya makabila ambayo watu wake wanaishi hapo ukiacha kabila la wasukuma ambao ndio wenyeji wa eneo hili, wapo pia watu wa jamii ya makabila ya Warongo, Wazinza, wanyiramba, wajaluo, Wajita na hata wakerewe ambapo

wengi ni wahamiaji tu, wamekuwa wakazi wa eneo hili kutokana na ama uhamiaji au kwa ajili ya biashara ndogondogo.

Majibu hayo yanafanana na mawazo ya Massamba na wenzake (2009) wanaodai kuwa, lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo hutumiwa na watu ambao idadi yake yakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 60. Idadi hiyo imekadiriwa kwa kuzingatia kwamba lugha hii inazungumzwa na takribani kila mtu katika Tanzania. tafiti ameshawishika kukubaliana na hoja hiyo ya watafitiwa wengi kwa kuzingatia uhalisi wao kuwa wana ujuzi au ufahamu wa kutosha katika lugha ya Kiswahili

Uchambuzi wa data katika lengo la kwanza la utafiti umedhihirisha kuwa, kwa jumla, majibu yaliyopatikana kwa njia ya mahojiano yanaendana na kushabihiana na yale majibu yaliyopatikana kwa njia ya dodoso na kwa kutumia zoezi la umilisi ambayo yameonesha. Kwa ufupi, wanafunzi wa darasa la saba wameonesha wana ujuzi na ubobezi katika lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika vipengele ambavyo mtafiti amewapima.

4.3 Kutathmini Kiwango cha Ubobezi wa Kiswahili Dhidi ya Sifa za Lugha ya Kufundishia Shule za Msingi

Madhumuni mahususi ya pili ya utafiti huu yalikuwa ni kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia katika shule za msingi.

Lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa kutolea elimu kwa taifa nzima au sehemu ya taifa na kwa kiwango maalum cha elimu au kwa viwango vyote vya elimu. Hoja hiyo inaungwa mkono na Msanjila na wenziwe (2009) waliposema kwamba lugha ya

kufundishia ni lugha inayotumiwa kutolea maarifa katika mfumo wa elimu. Lugha hiyo ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa mawasiliano katika elimu ya msingi kwa umma, kubuni na kuendeleza maarifa. Wanaendelea kueleza kuwa lugha ni chombo cha kuwapa watu uwezo na nguvu za kiutamaduni. Kwa mtazamo wao lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi.

4.3.1 Ubobezi Uliopimwa Dhidi ya Sifa za Lugha ya Kufundishia

Baada ya uchambuzi wa data zilizokusanywa kwa watafitiwa wa utafiti katika lengo mahususi la kwanza tathimini inaonesha kwamba, katika kipengele cha ufahamu wa wanafunzi katika kutambua na kubaini aina za maneno matokeo yanaonesha kuwa wanafunzi wana uwezo wa kutambua na kubaini aina za maneno ya lugha ya Kiswahili, matokeo yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya watafitiwa, sawa na asilimia 87, waliweza kubaini na kutambua aina za maneno katika sentensi ukiangalia uwezo huo walionao wanafunzi unawiana na sifa ya lugha kufundishia.

Mjuzi wa lugha ya kufundishia anauwezo wa kuzifahamu vyema sheria za kiisimu za lugha yake ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutambua aina mbalimbali za sentensi, kutambua aina za maneno ya lugha yake, pia kutambua sentensi sahihi na ambazo sio sahihi zikiwa zimeandikwa au kuzungumzwa. Kwa mujibu wa Chomsky (1965), umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki na othografia, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia

lugha; ni lazima awe na uwezo wa kiutendaji katika lugha husika yaani awe na uwezo wa kutumia lugha ile katika miktadha tofauti ya kijamii kwa usahihi.

Sifa nyingine ya lugha ya kufundishia inapaswa iwe ni lugha yenye kufahamika kwa wanafunzi na pia kwa walimu. Kama matokeo ya utafiti yanavyoonesha katika lengo mahususi la kwanza katika kipengele cha Sababu zinazochangia watafitiwa kuwa na ufahamu katika lugha ya Kiswahili. majibu toka kwa wanafunzi wengi sawa na asilimia 86, walisema kwa sababu Kiswahili kinatumika muda mwingi wa maongezi ya watafitiwa wanapokuwa shuleni baina yao na wanafunzi wengine na baina yao na walimu wao wakati wa ujifunzaji na ufundishaji aidha mawasiliano yote rasmi yanayofanyika shuleni , lugha ya Kiswahili ndio lugha itumikayo katika kutolea matangazo na maelekezo shuleni.

Senkoro (2004) anasema kuwa, lugha ifaayo kufundishia ni ile inayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi. Vile vile Rubagumya (2003) anadai kwamba, ufundishaji unaotumia lugha inayofahamika baina ya walimu na wanafunzi huleta ufanisi wa kutosha kwa sababu wanafunzi watajua jinsi ya kutumia maarifa ya kidhanifu katika taarifa mpya. Rubagumya (keshatajwa) anaendelea kudai kwamba, lugha inapokuwa ni ile iliyozoeleka kwa wanafunzi na ambayo walimu wanaimudu vyema huuleta uelewa mzuri wa dhana ya somo linalofundishwa.

Katika kipengele cha Ujuzi au ufahamu wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili matokeo yanaonesha kuwa wanafunzi wote waliohojiwa walisema wana ufahamu wa lugha ya Kiswahili, ukiangalia uwezo huo walionao wanafunzi unawiana na sifa

ya lugha ya kufundishia kama anavyosema, Halliday (1973) kuwa, lugha ya mawasiliano katika jamii ndiyo ifaayo kuwa lugha ya kufundishia kwa kuwa ndiyo lugha ambayo wanafunzi wanaifahamu vizuri. Lugha ya mawasiliano katika jamii inapopewa dhima ya kufundishia hukua na kuweza kueleza nyanja mbalimbali za maarifa. Sifa hizo zinabebwa na lugha ya Kiswahili na kwa hali hiyo inastahili kupewa kipaumbele cha kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya vyuo vya kati na vyuo vikuu. Fauka ya hayo, kwa sababu thamani na majukumu yanayotekelezwa na lugha yoyote katika jamii ya wingi lugha huathiri mielekeo na tabia za wanajamii katika kujifunza, kuithamini na kuitumia lugha hiyo.

Kwa mujibu wa Prah (2003), lugha ya kufundishia ni ile yenye athari kubwa katika mfumo wa elimu; ni nyenzo itumikayo kujenga mfumo thabiti wa elimu na huwa na nguvu na mamlaka kwa kuwa dhana kuu za elimu tayari zimo kwenye lugha hiyo ya asili, au ya karibu, kama kilivyo Kiswahili kwa Watanzania wengi. Lugha ya kufundishia ni lugha ambayo ina sifa ya kutumika katika miktadha mbalimbali katika jamii kama vile katika shughuli za kiserikali, shughuli za kisiasa, shughuli za kijamii kama vile misiba, harusi na shughuli za kidini. Miongoni mwa sababu walizosisema wanafunzi juu ya ujuzi wao katika lugha ya Kiswahili walisema kuwa wao wanakitumia Kiswahili katika miktadha mbalimbali katika maisha yao, hoja hii inaungwa mkono na Hymes (1972), alipohoji kuwa lazima kila mzugumzaji wa lugha aweze kufahamu jinsi ya kutumia lugha husika katika miktadha mbali mbali ya kijamii. Kama tulivyoona katika lengo la kwanza kuwa wanafunzi waliweza kutambua na kubaini msamiati, matumizi sahihi ya njeo na hata upatanisho sahihi wa kisarufi sifa hii inlandana na maelezo ya mwanaisimu, Hymes alipokubaliana na

Chomsky (1965) kuwa ni jambo la kimsingi kwa kila mzungumzaji wa lugha kuwa na umilisi au ujuzi wa kiisimu (sheria za lugha) wa lugha husika.

Lugha ya kufundishia kawaida huwa na kanuni na misingi maalumu ya lugha ambayo huifanya lugha hiyo iwe tofauti na lugha nyingine ambazo kanuni na misingi hiyo watumiaji wake ambao wanaumilisi wa lugha lazima wazijue kanuni na misingi hiyo. Hoja hii inafafanuliwa na Lucius (1978) ambaye anamini kwamba, kanuni na misingi ya lugha ndizo zinazotawala lugha za walimwengu wote kwa ujumla. Kila lugha ina kanuni na misingi maalumu inazozihusu lugha fulani tu ambayo huifanya lugha hiyo iwe tafauti na lugha zingine. Misingi na kanuni hizo maalumu zinakuwa pia katika lugha yetu ya Kiswahili. Mfano katika matumizi ya njeo. Njeo ni asasi muhimu katika mjengeko wa maneno. Huweka bayana utofauti wa wakati ambao tendo hutokea. Yaani, njeo hufahamisha wakati tendo lilipotokea, linapotekea au litakapotekea. Waandishi wengi wa sarufi ya Kiswahili wamezibainisha njeo katika namna tatu. Yaani, kuna njeo ya wakati tulionao yenye kuwakilishwa na mofimu ‘-na-’, njeo ya wakati ujao inayowakilishwa kwa ‘-ta-’, na njeo ya wakati uliopita ambayo huwakilishwa kwa ‘-me-’ iwapo wakati uliopita ni muda mfupi, na kwa ‘-li-’ iwapo umepita wakati mrefu. Lengo la kwanza katika eneo hili la njeo, matokeo yanaonesha kuwa wanafunzi wengi sawa na asilimia 95 waliweza kutambua sentensi ambazo ziko katika nyakati mbalimbali na pia wanafunzi wote sawa na asimilia mia moja waliweza kutunga sentensi mbalimbali zikiwa katika nyakati tofauti tofauti, matokeo haya yanadhihirisha kuwa wanafunzi wana ufahamu mzuri katika lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia.

Lugha ya kufundishia huwa ni lugha ambayo ina msamiati wa maneno mbalimbali ambayo hutumika wakati wa mawasiliano na mzawa wa lugha hiyo anakuwa na uwezo wa kutambua na kubaini msamiati wa lugha hiyo. Katika kufanikisha mawasiliano, lugha huhusishwa na kutegemea msamiati, semi pamoja na viziada lugha. Bolinger na Seas (1981) wanaeleza kuwa uwezo wa binaadamu wa kujifunza kuimudu na kuitumia lugha kwa ufaafu hujitokeza katika utumizi wa maneno mbalimbali ya lugha hiyo.

Msamiati hutumiwa kutaja vitu na kurejelea hali anuwai. Matumizi huongozwa, huelekezwa na kudhibitiwa na kaida pamoja na maadili ya jamii husika. Wanafunzi walengwa wa utafiti huu ufaulu wao katika kipengele cha msamiati kinaenda na sifa hii kutokana na matokeo ya utafiti ambapo wanafunzi walionesha kukimudu kipengele hiki. Matokeo yaliyopatikana kutokana na utumizi wa msamiati katika sentensi yanaonesha kuwa wanafunzi wengi sawa na asilimia 87 waliweza kubaini na kutumia kwa usahihi. Matokeo haya yanamshawishi mtafiti kusema kuwa tathimini ya wanafunzi inaonesha kuwa wana ufahamu katika kiswahili kama lugha ya kufundishia. Dhana zinazoashiriwa na maneno /msamiati hutarajiwa kutambulika na kubainika na wanajamii. Hudson (1995) anaeleza kuwa kama mfumo nasibu, lugha huhitaji urudifu wa neno/ msamiati linaloashiria dhana fulani ili kulizoeshwa kwa matumizi hayo.

4.3.2 Ushahidi wa Ubobezi wa Kiswahili katika mitihani ya ndani

Kwa kutumia mbinu ya usomaji wa nyaraka/machapisho, Mtafiti alipitia matokeo ya watafitiwa hao 20 toka kila shule kuona ufaulu wao kwa masomo matano ambayo ni

somo la Kiswahili, somo la maarifa ya jamii, somo la sayansi, Hisabati na somo la kiingereza yanayofundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili ili kuona ufaulu wao wa mitihani ya ndani ya shule iliyofanyika mwezi wa sita. Lengo likiwa ni kufanya tathimini na kulinganisha ufahamu wao uliobainishwa katika utafiti huu watafitiwa wakati wa kujibu maswali ya usaili, hojaji na upimaji uliofanyika kwa kutumia zoezi la umilisi ili kuona ubobezi au ufahamu walionao watafitiwa unalandana na ufaulu wao katika mitihani yao.

4.3.2.1 Ufaulu wa somo la Kiswahili

Katika somo la Kiswahili, matokeo ya ufaulu wao wa mtihani wa muhula wa kwanza ulikuwa kama ulivyooneshwa katika jendwali.

Jedwali 4.11: Matokeo ta Ufaulu wa Wanafunzi Kwa Somo la Kiswahili

Shule	Idadi	Daraja la ufaulu			
		A	B	C	D
Bufunda	20	16	3	1	-
Buyagu	20	15	5	-	-
Kashishi	20	19	1	-	-
Kasungamile	20	14	4	2	-
Nyakamwaga	20	18	2	-	-
Jumla	100	82	15	3	-

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.11 linaonesha kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa, sawa na asilimia 82, walipata ufaulu wa daraja ‘A’ katika mtihani wa muhula wa kwanza katika somo la Kiswahili, asilimia 15 walipata ufaulu wa daraja ‘B’ huku asilimia 3 wakipata daraja ‘C’ na hakuna mwanafunzi yeyote aliyepata daraja ‘D’. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili ni mzuri na hivyo wanauelewa katika somo hili ambalo hufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili, kama wanavyosema Backman na Palmer (1996) uwezo wa lugha anaozaliwa nao mtu kama vile tabia za kijumuiya, ujuzi au maarifa ya mada inayozungumzwa, utambuzi na uwezo alionao mtu katika lugha huathiri uwezo wa kutumia lugha katika mawasiliano na hivyo kufanya ufaulu wake kuwa mzuri.

4.3.2.2 Ufaulu wa Somo la Maarifa ya Jamii

Mtafiti alipata nafasi ya kuona na kuchukua taarifa za ufaulu wa wanafunzi 20 kwa kila shule wale ambao walifanyiwa usaili na hojaji wakati wa ukusanyaji wa data katika lengo mahususi la kwanza. Katika somo maarifa ya jamii matokeo ya watahiniwa hao yalikuwa kama ifuatavyo katika jedwali hapo chini.

Jedwali 4.12 : Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi Kwa Somo la Maarifa ya Jamii

Shule	Idadi	Daraja la Ufaulu			
		A	B	C	D
Bufunda	20	12	5	3	-
Buyagu	20	12	7	1	-
Kashishi	20	11	4	5	-
Kasungamile	20	14	5	1	-
Nyakamwaga	20	17	2	1	-
Jumla	100	66	23	11	-

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.12 linaonesha kwamba asilimia 66 ya watafitiwa, walipata ufaulu wa daraja ‘A’ katika mtihani wa muhula wa kwanza katika somo la maarifa ya jamii, asilimia 23 walipata ufaulu wa daraja ‘B’ na asilimia 11 wakipata daraja ‘C’ na hakuna mwanafunzi yeyote aliyepata daraja ‘D’. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika somo la maarifa ya jamii ni mzuri na hivyo wanaulewa katika somo hili ambalo hufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

4.3.2.3 Ufaulu wa somo la Hisabati

Katika somo la Hisabati, matokeo yao ya ufaulu wa mtihani wa muhula wa kwanza ulikuwa kama ulivyooneshwa katika jedwali. Wakati wa mitihani hiyo wanafunzi 03 ambao ni kutoka shule ya msingi Bufunda mwanafunzi 01 na wengine 02 wa shule ya msingi Kasungamile hawakufanya mtihani wa muhula wa kwanza kutokana na sababu ambazo walimu wao wanazijua hivyo hawakuwa wamewekewa alama za ufaulu wao.

Jedwali 4.13: Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi kwa Somo la Hisabati

Shule	Idadi	Waliofanya	Daraja la Ufaulu			
			A	B	C	D
Bufunda	20	19	09	06	04	-
Buyagu	20	20	14	05	01	-
Kashishi	20	20	09	08	03	-
Kasungamile	20	18	08	08	02	-
Nyakamwaga	20	20	12	05	03	-
Jumla	100	97	53	32	12	-

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.13 linaonesha kwamba asilimia 97 ya wanafunzi waliolengwa kufanyiwa utafiti walifanya mtihani wa muhula wa kwanza kwa somo la Hisabati na wanafunzi 3 sawa na asimilia 3 ya walengwa hawakufanya mtihani. Matokeo yao yanaonesha kuwa wanafunzi 53 sawa na asilimia 55 ya wanafunzi waliofanya mtihani walipata ufaulu wa daraja ‘A’ katika somo la Hisabati, wanafunzi 32 sawa na asilimia 33 walipata ufaulu wa daraja ‘B’ na wanafunzi 12 sawa na asilimia 12 wakipata daraja ‘C’ na hakuna mwanafunzi yeyote aliyepata daraja ‘D’. Matokeo haya yanaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika somo la Hisabati ni mzuri kwa kuwa asilimia 55 walipata ufaulu wa daraja ‘A’ na hivyo wanaulewa katika somo hili ambalo hufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

4.3.2.4 Ufaulu wa Somo la Sayansi

Mtafiti alipata nafasi ya kuona na kuchukua taarifa za ufaulu wa wanafunzi 20 kwa kila shule wale ambao walifanyiwa usaili na hojaji wakati wa ukusanyaji wa data katika lengo mahususi la kwanza. Katika somo Sayansi matokeo ya watahiniwa hao yalikuwa kama ifuatavyo katika jedwali hapo chini.

Jedwali 4.14: Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi Kwa Somo ya Sayansi

Sn	Shule	Idadi	Daraja la Ufaulu			
			A	B	C	D
1	Bufunda	20	13	03	01	03
2	Buyagu	20	11	05	03	01
3	Kashishi	20	12	04	02	02
4	Kasungamile	20	14	04	02	-
5	Nyakamwaga	20	13	02	04	01
	Jumla	100	53	28	12	07

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.14 linaonesha kwamba wanafunzi 53 sawa na asilimia 53, walipata ufaulu wa daraja ‘A’ katika mtihani wa muhula wa kwanza katika somo la Sayansi, asilimia 28 walipata ufaulu wa daraja ‘B’, asilimia 12 wakipata daraja ‘C’ na wanafunzi 7 sawa na asilimia 7 walipata ufaulu wa daraja ‘D’. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika somo la Sayansi yalikuwa wastani na hivyo wanaulewa katika somo hili ambalo hufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

4.3.2.5 Ufaulu wa Somo la Kiingereza

Mtafiti alipata nafasi ya kuona na kuchukua taarifa za ufaulu wa wanafunzi 20 kwa kila shule wale ambao walifanyiwa usaili na hojaji wakati wa ukusanyaji wa data katika lengo mahususi la kwanza. Katika somo la Kiingereza ambalo somo hili hufundishwa kwa lugha ya kiingereza. Matokeo ya watahiniwa hao yalikuwa kama ifuatavyo katika jedwali hapo chini.

Jedwali 4.15 : Matokeo ya Ufaulu wa Wanafunzi kwa Somo la Kiingereza

Shule	Idadi	Daraja la Ufaulu			
		A	B	C	D
Bufunda	20	0 3	0 6	0 6	0 5
Buyagu	20	0 4	0 5	0 4	0 7
Kashishi	20	0 3	1 0	0 4	0 3
Kasungamile	20	-	0 9	0 3	0 8
Nyakamwaga	20	0 5	1 0	0 5	-
Jumla	100	1 5	4 0	2 2	2 3

Chanzo: taarifa za tasinifu, (2019)

Jedwali 4.15 linaonesha kwamba wanafunzi 15 sawa na asilia 15 watafitiwa walipata ufaulu wa daraja ‘A’ katika mtihani wa muhula wa kwanza katika somo la Kingereza, wanafunzi 40 sawa na asilimia 40 walipata ufaulu wa daraja ‘B’ wanafunzi 22 sawa na asilimia 22 wakipata daraja ‘C’ na mwanafunzi 23 sawa na asilimia 23 walipata daraja ‘D’. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiingereza ambalo hufundishwa kwa lugha ya Kiingereza sio mzuri kwani waliopata ufaulu wa daraja ‘A’ wako wachache sana huku wanafunzi wengi wakiwa katika ufaulu wa kiwango cha daraja ‘B’ na asilimia 23 walipata daraja ‘D’ ambalo sio zuri. Matokeo haya ya somo la Kiingereza yanamshawishi mtafiti kusema kuwa ufaulu huo duni umesababishwa na matumizi ya lugha ambayo sio lugha ya kufundishia kwa shule za msingi. Kutokana na Backman na Palmer (1996) uwezo wa lugha anaozaliwa nao mtu kama vile tabia za kijumuiya, ujuzi au maarifa ya mada inayozungumzwa, utambuzi na uwezo alionao mtu katika lugha huathiri uwezo wa kutumia lugha katika mawasiliano na hivyo kuathiri hata ufaulu wake.

Kwa ujumla, tathimini ya matokeo ya watafiti katika lengo la kwanza ambayo yalionesha walifanya vizuri sana karibu vipengele vyote vilivyofanyiwa upimaji kwa wanafunzi, ambavyo ni ujuzi wa wanafunzi katika kutambua na kubaini aina za maneno, uwezo wa wanafunzi katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha, matumizi ya muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi, utambuzi wa matumizi ya nafsi katika tungo, ufahamu wa matumizi ya njeo, uelewa wa watafitiwa katika utumizi wa lugha na utumizi wa lugha katika mazingira mbalimbali. Kutokana na uchambuzi wa data uliofanywa, asilimia kubwa kwa kila kipengele wanafunzi walikuwa na ujuzi nao, matokeo hayo yanamshawishi mtafiti

kusema kuwa wanafunzi wa darasa la saba wana ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia lakini pia katika lengo la pili la kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia shule za msingi kuona kama kiwango cha ubobezi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi kinalandana na sifa tarajali za ubobezi katika lugha ya kufundishia shule za msingi. Matokeo ya ufaulu alioukata mtafiti ni kigezo muhimu ambacho kinaonesha na kumpa ushawishi wa kutoa tathmini yake kuwa ni dhahiri wanafunzi wana kiwango cha ubobezi wa lugha ya Kiswahili na kinalandana na sifa tarajali za ubobezi katika lugha ya kufundishia shule za msingi.

4.4 Hitimisho

Sura hii imewasilishwa na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu ya zoezi la umilisi, hojaji na mahojiano. Uwasilishaji wa uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti huu na umeongozwa na mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi. Aidha, Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) ilizotumika katika utafiti huu imesaidia kuchanganua data za utafiti na kuweka wazi majibu ya maswali ya utafiti huu. Nadharia hii imetumika tokea hatua ya ukusanyaji wa data mpaka hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data Aidha, utafiti umejadili ufahamu wa lugha walionao wanafunzi wa darasa la saba kwa shule za msingi, Matokeo hayo yameonyesha kwa jumla kwamba wanafunzi ni wabobezi katika lugha ya Kiswahili. Sura inayofuata baada ya sura hii, inawasilisha muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo

SURA YA TANO

MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu kuhusu upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi. Sehemu ya kwanza ya sura hii inahusu muhtasari, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo.

5.2 Muhutasari wa Utafiti

5.2.1 Muhutasari wa Jumla

Utafiti huu ulikusudia kupima ufahamu wa wanafunzi katika lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi kwa kutumia mfano wa shule za kata ya Nyakamwaga wilayani Geita. Ili kufanikisha lengo kuu, utafiti ulikuwa na madhumuni mahsusi mawili ambayo ni kupima ubobezi wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa shule za msingi na Kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili dhidi ya sifa za lugha ya kufundishia shule za msingi. Utafiti huu uliwashirikisha watafitiwa 100 waliotumika kama wawakilishi wa utafiti huu. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya zoezi la umilisi, usaili na hojaji.

Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia madhumuni mahsusi ya utafiti na ulitumia mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Utafiti huu ulifuata maadili ya utafiti na uliongozwa na nadharia mbili ya kwanza ni Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) ambapo mtafiti alitumia nadharia hii katika kuangalia jinsi wanafunzi wanavyoweza kufuata sheria za lugha, yaani

uwezo wa mzungumzaji wa kuzifahamu vyema sheria za lugha, kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo.

Nadharia ya pili ni nadharia ya uwezo wa mawasiliano wa lugha ya Bachman na Palmer (1996), Mtafiti alitumia nadharia hii kuangalia uwezo wa wanafunzi katika utendaji wa lugha, yaani jinsi ya kutumia lugha ipasavyo katika miktadha tofauti ya kijamii kwa mfano kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua na kubaini aina za maneno katika sentensi pia kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha vile vile ujuzi wa watafitiwa katika sarufi ya lugha kuhusu usanifu wa lugha na muundo wa sentensi, matumizi ya maneno katika nyakati mbalimbali na matumizi wa lugha katika mazingira mbalimbali, Kutokana na upimaji ulifanyika katika vipengele hivyo, Matokeo yamedhihirisha kuwa, Ufahamu wa wanafunzi katika katika vipengele hivyo upo katika kiwango cha juu kwa maana kuwa wameboba katika lugha ya Kiswahili na ni wamilisi wa lugha ya Kiswahili.

5.2.2 Muhutajari wa Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu wanafunzi walipimwa juu ya ujuzi na ubobezi walionao katika lugha ya kiswahili, wengi waliweza kujibu maswali ya utafiti kwa ufasaha na kwa usahihi na kudhihirisha kuwa wanaufahamu mzuri wa lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa wanafunzi wana ufahamu katika lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi baada ya kujibu vizuri maswali ya utafiti yaliyokuwa yanapima ufahamu wao wa lugha ya Kiswahili katika vipengele tofauti tofauti. Kwa upande wa kipengele cha ubobezi wa Kiswahili kama

lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa shule za msingi matokeo ya watafitiwa juu ya matumizi wa lugha yameonesha kuwa wana uwezo wa kubaini sentensi ambazo ziko sahihi na ambazo haziko sahihi kimuundo katika lugha ya Kiswahili.

Katika kipengele cha Uwezo wa wanafunzi katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha na pia Ujuzi wa watafitiwa katika sarufi ya lugha kuhusu muundo wa sentensi. Watafitiwa wamebainika kuwa wana ufahamu mzuri katika matumizi sahihi ya msamiati na usanifu wa lugha na hivyo wana ufahamu katika lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia aidha wanafunzi waliweza kujibu maswali yaliyohusiana na muundo wa sentensi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Hiki ni kiashiria tosha kuwa watafitiwa wetu wana ufahamu mzuri wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na wana ujuzi wa kutosha katika lugha ya Kiswahili. Katika kipengele cha Ufahamu wa wanafunzi katika kutambua na kubaini aina za maneno, Wanafunzi wengi waliweza kubaini na kutambua aina za maneno katika sentensi.

Kwa ujumla Utafiti huu ambao ulikuwa na lengo la kupima ufahamu walionao wanafunzi wa darasa la saba, umebaini kuwa wanafunzi wana ubobezi na umilisi katika lugha ya Kiswahili.

5.3 Hitimisho

Kwa umilisi walionao wanafunzi ni dhahiri wataweza kupandisha kiwango cha taaluma yao kwa masomo yanayofundishwa kwa lugha ya Kiswahili, wanafunzi watatumia uwezo na ujuzi wa kubuni na kung'amua mambo mbalimbali ya

kitaaluma. Kiswahili ni tunu ya taifa letu hivyo kipewe kipaumbele kuwa lugha ya kufundishia sii tu kwa elimu ya msingi kitumike hata elimu ya sekondari na vyuo vya kati ili kuwapa urahisi walimu na wanafunzi kuwasiliana na kuelewa masomo ya sekondari na vyuo vya kati wakati lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kuwa na ufahamu wa kuwasiliana kimataifa.

5.4 Mapendekezo

5.4.1 Mapendekezo ya Jumla

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kwamba serikali ione uwezekano wa kuipa hadhi lugha ya Kiswahili na kuirasimisha kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na vyuo vya kati kwa lengo la kukuza viwango vya ufahamu na ufaulu, uchumi, kuendeleza utamaduni wa taifa na kuimarisha lugha ya Kiswahili.

5.4.2 Mapendekeo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulijikita katika upimaji wa ufahamu wa wanafunzi katika lugha kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za msingi katika wilaya ya Geita vijijini kwa shule tano za kata ya Nyakamwaga. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti kama huu ufanyike zaidi katika maeneo mengine zaidi ya walaya ya Geita ili kulinganisha matokeo ya ufahamu wa wanafunzi katika lugha ya kufundishia. Pili, mtafiti hakuvifanyia kazi vipengee vyote vya mtaala wa elimu ya msingi pamoja na muhutasari wa Kiswahili kwa darasa la saba kama vile lugha za kisanii, ufahamu na ufasaha wa usomaji. Mapendekezo ya mtafiti ni kwamba tafiti zingine zinaweza kufanyika juu ya upimaji katika lugha za kisanii,

ufahamu au kuwapima wanafunzi juu ya ufasaha wao katika usomaji wa matini na hadithi mbalimbali wakizingatia alama za uandishi wa habari.

MAREJEO

- Adam, J. na Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies*, Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Babyegeya, E. (1998). *Test and Measument*. Dar es Salaam: Open University of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
- Bachman, L.F na Palmer, A.S (1996). *Language Testing in Practice*. Buck: Oxford University Press.
- Bhaiji, A. F. (1976). The Medium of Instruction in Our Secondary Schools. A Study Report in Education and Devolopment. Department of Education, University of Dar es Salaam. Dar es Salaam, Tanzania
- Brock-Utne, B. (2000). *Whose Education for All? Re-colonization of the African Mind*. New York: Falmer press.
- Brock-Utne, Desai Z.and Qorro, M.A.S. (eds), (2003). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*.Dar es Salaam: E& D publishers
- Brock-Utne, B. (2003). Language Question in Africa in the Light of Globalisation, Social Justice and Democracy. *International Journal of peace studies*, vol. 8 uk 2
- Brock-Utne B., Desai, Z. and Qorro, M.A.S. (2005). *LOITASA Research in Progress. Language of Instruction in Tanzania and South Africa*.Dar es Salaam: KAD Associates.
- Brock-Utne, B. (2006). *The Continued Battle over Kiswahili as the Language of Instruction inTanzania*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota
- Canale, M. na M. Swain (1980). *Theoretical Bases of Communicative Approaches to Second Language Teaching and Testing. Applied Linguistics*. London:

Longman.

Canale M. na Swain M.(1980) Theoretical base of Communication Approach to Second language teaching and testing *Applied linguistics*, Vol. 1, pp. 1-47.

Canale, M. (1983). "From Communicative Competence to Communicative Language Pedagogy" In: Richards J, Schmidt R (eds). *Language and Communication*. London: Longman.

Chimera, R. (1998). *Kiswahili Past, Present and Future Horizons*, Nairobi: OUP

Chiragdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: O.U.P.

Chomsky. N (1957). *Syntactic Structure Cambridge*: Cambridge University press.

Chomsky, N. (1976). *Reflections on Language*. London: Temple Smith.

Criper, C. & Dodd, W. (1984). *Report on the Teaching of English Language and its Use as a Medium of Education in Tanzania*. The British Council. Dar es Salaam, Tanzania.

Desai, C. and Qorro, M.A.S. (eds) (2003). *The language of Instruction in Tanzania and south Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E&D Publishers.

Crystal D.(1997), *The Cambridge Encyclopedia of language*. London: Cambridge university press

Ellis, R. (1994). *The study of Second Language Acquisition*. London: Oxford University Press

Enon, C. J. (1998). *Education Research and Measurement*, Department of Distance Education, Makerere University, Uganda.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

- Halliday, M. A. K. (1973). *Exploration in the Function of Language*. London: Edward Arnold.
- Heine, B. (1992). "Language Policies in Africa". In: R. Herbert (ed.), *Language and Society in Africa. The Theory and Practice of Sociolinguistics*, pp. 23–35. Cape Town: Witwatersrand University Press.
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2011). *Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi: Sera ya Elimu na Mafunzo 2010*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Kamugisha, D. J. na Mateng'e, F.J. (2004). Politics of Curriculum Making: A Quandary to Quality Education in Tanzania? *International Journal of social science and Enterpreurship* 1pg 9.
- Kaplan, R. na Baldauf, R. (1997). *Language Planning from Practice to Theory*. Clevedon: Multilingual matters
- Kombo, D. and D. Tromp (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication Africa.
- Kothari, R. C. (1990). *Reseach Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi. New Age International (P) Limited.
- Kothari, C. R. (2004). *Research methodology Methods and Technique (Second Revised Edition)*. New Delhi: New age International Publishers.
- Kothari, R. C. (2008), *Research Methodology; Methods*. New Delhi New Age International Publishing LTD
- Kothari R. (2012). *Research Methodology: Methods and Techniques (Second Revised Edition)*. New Delhi: New age International Publishers.
- Koul, O. N. (2008). *Modern Hindi grammar*. Springfield, VA 22150, USA: McNeil Technologies, Inc. <http://www.iils.org/pdf/ModernHinduGrammar.pdf>

- Koul L. (2009). *Methodology of Educational Research*, fourth Revised and Enlarge Edition. Inda Vikas publishing House PVT Ltd: New Delhi India.
- Krashen, S. D. na Tracy D. T. (1983), *The Natural Aproach Language Acquisition in The Classroom*. Oxford: Pergamon Press.
- Massamba D. (1989). “An Assessment of the Development and Modernization of Kiswahili Language in Tanzania”. In F. Coulmas (Ed) *Language Adaptation*. London: Cambridge University Press.
- Massamba, D. Kihore, Y. & Hokororo, J. (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Sekondari na Vyuo*, Dar –es –Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
- Mekacha.R.D.K. (1995) Kwa nini Kiingereza Bado ni Lugha ya Kufundishia Elimu ya Juu Tanzania? *Kioo cha lugha, Journal of the institute of kiswahili studies,university of Dar es salam*.
- Mekacha, R. D. K. (1997). Language as a Determinant of the Quality of Education.A Rejoider, *Journal of Linguistics and Language in Education* Vol 3:95-105.
- Mekacha, R. (2000). Isimu jamii-Nadharia na muktadha wa Kiswahili.Minoocity : Osaka university of Foreign studies.
- Mochiwa, Z. S. M. (1979).The Impact of Kiswahili on Ethnic Languages.A Case Study of Handeni District.Unplished M.A. Thesis: University of Dar es Salaam.
- Mlama, P. & Matteru, B. (1978). *Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia katika Elimu ya juu*. Dar es Salaam: BAKITA.
- Mlama, P. na Matteru, M. (1980) Haja ya kutumia Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia katika Elimu ya Juu. *Lugha Yetu,juzuu ya 35 na juzuu ya 36*.

- Mligo, S.E (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam. Ecumenical Gathering (EGYS).
- Msanjila, Y. P. (1998). Uzoefu wa kutumia Kiswahili kama Lugha ya kufundishia katika Vyuo vya Ualimu nchini Tanzania. *Journal of Linguistics and Language in Education*, Vol.3, pp 75-95.
- Msanjila, Y.P. (2004). "Kiswahili kitumike kufundishia shule za sekondari na Elimu ya juu Tanzania". In: Y.M Kihore and A.R. Chuwa (eds.), *Kiswahili katika karne ya Ishirini na moja*. Dar es Salaam. TUKI: Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Kurasa 40 –49.
- Msanjila, Y. P. (2007). Utumiaji WA Kiswahili Na Lugha za Jamii. Kijinsia nchini Tanzania. *Nordic Journal of African Studies*, Vol.3, No.6, pp. 34-51.
- Msanjila Y. P. (2009). Haja ya Kuwa na Sera Toshelevu ya Lugha Tanzania: Uzoefu Na Changamoto. *Mulika Juzuu*. 28, kur. 62-71.
- Msanjila, P. Y na wenzake (2009). *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam. TUKI.
- Msanjila, P. Y na wenzake (2011). *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam. TUKI.
- O-saki, K. M. (2003). Evaluation of Lead Teacher Training Institutes in Ethiopia. A Consultancy Report Prepared for UNESCO. Paris: UNESCO
- Peterson, R. (2006). *The use of an African Language as Language of Instruction at University level. The Example of Kiswahili Department at the University of Dar es Salaam in Tanzania*. Oslo: Institute of Educational Research.
- Pons, V. (1992). *Introduction to Social Research*. Dar-es-salaam : Dar-es-salaam University Press.

- Puja, G. K.(2003).”Kiswahili and Higher Education in Tanzania. Reflections Based on a sociological study from three Tanzanian university Campuses”. In Brock-Utne, Birgit, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds), *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E& D publishers
- Prah, K. K. (2003). “Going Native: Language of Instruction for Education, Development and African Emancipation”. In B. Brock Utne, Z Depai and Qorro. (Eds). *Languages of instruction in Tanzania*. Dar-es Salaam: E & D Limited.
- Qorro, M. A. S. (2005). “Parents’ Views on the Medium of Instructions in post-Primary Education in Tanzania”. In: B.Brock-Utne, Desai Z.and Qorro, M.A.S. (eds) *LOITASA Research in progress*. Dar es Salaam. KAD Associates.
- Qorro M. A. S. (2006). Does Language of Instruction Affect Quality of Education? University of Dar es Salaam, Haki Elimu working Papers.Dar es Salaam
- Richard J.C na Rodgers T.S (2001), *Approaches and Methods in Language Teaching*. New York: Cambridge University press.
- Rocha, M.C (2011) *Kiswahili Past Present and Future Horizons*, Nairobi University Press
- Rubagumya, C. M. (1991), "Language promotion for educational purposes: the example of Tanzania", in Legère, K. (ed.), *The role of language in literacy programmes with special reference to Kiswahili in eastern Africa*. Bonn: Deutsche Stiftung für Internationale Entwicklung, 198-215.
- Rubagumya, C.M (2003). “English Medium Primary Schools in Tanzania. A new

- Linguistic Market in Education?” In: Birgit Brock-Utne, Zubeida, D. and Qorro, M.A.S. (eds), *Language of Instruction in Tanzania and South Africa*. Dar es Salaam: E&D Limited.
- Rubanza , Y. I (2013) *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo*, Dar es salam: Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.
- Rubin, J. & Jenudd, B. H. (Eds) (1971). *Can Language be Planned? Sociolinguistic Theory and Practice for Developing Nations*. Honolulu: Honolulu University Press.
- Sengo, T.S.Y. (1987) Towards Maturity in Kiswahili Scholarship. *Kiswahili Juzuu* 54, kur 215-224
- Sengo Y. (1995). Hali ya kutatanisha ya Kiswahili hivi leo “Afrika mashariki “ ;makala kwa ajili ya kongamano la nane la kiswahili chuo kikuu cha Bayreath. tarehe 26 na 27 mei 1995
- Senkoro, F. (2004). “The Role of Language in Education and Poverty Alleviation: Tool for Access and Empowerment”, in Galabawa J. and Narman, A. (Eds.). *Education Poverty and Inequality* Dar es Salaam: KAD Associates
- Taasisi ya elimu Tanzania (2005), *Mwongozo wa Tathimini na Upimaji*, Dar-es Salaam, Tanzania.
- Taasisi ya elimu Tanzania (2006), *Mwongozo wa Tathimini na Upimaji*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Tikolo, O. (2012). English Language In competency amongst Senior secondary school Graduates in Nigeria A-801: Education policy Analysis and Research utilization in comparative perspective, Harvard Graduate School of Education, December 12, 201.

- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- TUKI (2010). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press Vuzo.
- Trudgill, P. (1983). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. London: Penguin Book Ltd.
- UNESCO, (1953). *The Use of Vernacular Languages in Education*, Paris: UNESCO.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1996), *Muhtasari wa Kiswahili*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005), *Muhtasari wa Somo la Kiswahili*, Dar-es Salaam, Tanzania.
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2011), *Sera ya Elimu*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, (2014), *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Dar-es Salaam, Tanzania.
- Wizara ya elimu sayansi na teknolojia (2016), *Muhtasari wa somo la Kiswahili*, Dar-es Salaam, Tanzania.
- Whiteley, W.H. (1969), *Swahili: The Rise of National Language*. London: Methuen.
- Yoradi S.Y. (2013). *Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia Elimu Shuleni na Vyuoni*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (M.A. Kiswahili), Chuo kikuu Huria cha Tanzania.
- Zhou, M. and Sun, H. (2004). *Language Policy in the People's Republic of China: Theory and Practice Since 1948* [<http://www>].

utwente.nl/cw/theorieenoverzicht/ theory].

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO NA. 1: BAJETI

BAJETI YA KAZI YA UTAFITI

Sn	Maelezo	Gharama
1	Matayarisho ya uandishi wa pendekezo- Vifaa vya kuandikia kama vile madaftari, kalamu, rula	150,000/=
2	Huduma za komputa na intaneti	300,000/=
3	Gharama za usafiri kwa ajili ya kukutana na wadau	250,000/=
4	Matayarisho ya zana za kukusanya data Kutayarisha maswali ya usaili	100,000/=
5	Kukusanya data, Usafiri kwa ajili ya kufuata watafitiwa	250,000/=
6	Uchambuzi wa data	100,000/=
7	Uandishi wa ripoti	400,000/=
8	Usafiri wa kuwasilisha ripoti jijini Dar es Salaam	300,000/
9	Kuchapa na kutoa ripoti.	500,000/=
	Jumla kuu	2,350,000/=

**KIAMBATANISHO NA 3 : ZOEZI KWA AJILI YA WANAFUNZI LA
KUPIMA UFAHAMU WA LUGHA**

Taarifa za awali za wahojiwa

Jinsi me () ke ()

Darasa

Umri (miaka)

Jina la Shule

Kata

Wilaya

Mkoa

Tarehe

Chagua jibu sahihi kwa kuweka herufi ya jibu katika kisanduku ulichopewa.

1. “Yeye amefaulu mitihani yake vizuri”. Katika sentensi hii neno lipi limetumika kama kitenzi?

a) yeye

b) amefaulu ()

c) mitihani

d) yake

2. “Mnyama mkali amekamatwa leo.” Katika sentensi hii neno “mkali” limetumika kama aina gani ya neno ?

a) kielezi

b) kiwakilishi ()

c) kivumishi

d) kitenzi

3. “Kitabu changu ni cheusi, chako ni cheupe.” Neno “chako” ni aina gani ya neno ?

a) kivumishi

b) kiwakilishi ()

c) kielezi

d) kihusishi

4. “Siku ile ya maandamano kulikuwa na wa pikipiki”. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo ?

a) msururu

b) msurulu ()

c) msululu

d) musururu

5. Tulihudhuria kwenye ya kumuaga dada yetu.

a) tahadhari

b) taharuki ()

c) tafrija

d) frija

6. Kinyume cha kitenzi “paa” ni kipi?

a) Toweka

b) Elea ()

c) Shuka

d) Tua

7. “Hapa alipoishi chifu wa wanyaturu”

a) ndiko

b) ndimo ()

c) ndio

d) ndipo

8. Yeye ni kijana mdogo. Neno “yeye” lipo katika nafsi gani ?

a) Ya kwanza umoja

b) Ya tatu umoja ()

c) Ya pili umoja

d) Ya tatu wingi

9. Atakapomnyonya yule bata kwenye moto.

a) Atambanika

b) Anambanika ()

c) Amembanika

d) Alimbanika

10. “Walikotoka kuna mvua.” Sentensi hiyo ipo katika wakati gani ?

a) Wakati uliopo

b) Wakati uliopita ()

c) Wakati ujao

d) Wakati wa sasa

Asante kwa ushirikiano wako

KIAMBATANISHO NA. 4: MAHOJIANO KWA AJILI YA WANAFUNZI

Taarifa za awali za wahojiwa

Maswali kwa ajili ya wanafunzi

Taarifa za awali

Jinsi me () ke ()

Darasa

Umri (miaka)

Jina la Shule

Kata

Wilaya

Mkoa

Tarehe

Jibu maswali yafuatayo kwa usahihi.

1. Je unao ujuzi au ufahamu wa kutosha wa lugha ya Kiswahili?

.....

2. Kwa vigezo gani unajiona unao/huna huo ujuzi/ufahamu ?

.....

3. Taja sababu zinazochangia wewe kama mwanafunzi kuwa na ufahamu katika lugha ya kiswahili

.....

4 .Tunga sentensi moja moja kwa kila nyakati kwa kuzingatia mofimu ya waakati uliopewa

i) wakati uliopita mofimu –li-

.....

ii) wakati uliopo kwa kutumia mofimu –na-

.....

iii) Wakati ujao kwa kutumia mofimu –ta-

.....

Asante kwa ushirikiano wako.

KIAMBATANISHO NA. 5 : ZOEZI LA UMILISI WA LUGHA

Taarifa za awali za wahojiwa

Jinsi me () ke ()

Darasa

Umri (miaka)

Jina la Shule

Kata

Wilaya

Mkoa

Tarehe

Weka alama ya vema kwenye jibu ambalo ni sahihi:

1. Je, unapendelea kutumia lugha gani zaidi katika mijadala/majadiliano ya mada za masomo unayofundisha hapa shuleni ?

Kiswahili (), kiingereza (), kisukuma (), nyingine ()

Unapokuwa unafanya mawasiliano na walimu wako unatumia lugha gani ?

Kiswahili (), kiingereza (), kisukuma (), nyingine ()

Unapokuwa katika shughuli za nje ya darasa mfano katika michezo au shughuliza uzalishaji shuleni unatumia lugha gani?

Kiswahili (), kiingereza (), kisukuma (), nyingine ()

Weka alama ya vema mbele ya sentensi ambayo unadhani kuwa iko sahihi na alama ya kosa mbele ya sentensi ambayo unadhani haiku sahihi.

Nitakuja kwako ijumaa ijayo ()

Masanja aliondoka kesho ()

Ng'ombe wangu wamepotea ()

Viti hizi zimeharibika ()

Mwalimu aliyekuja jana ameondoka kesho asubuhi ()

Nimekuja hapa tangia asubuhi ()

Nimekuja hapa tangu asubuhi ()

Dada anamwandikiaga barua baba ()

Mapanya hawa wanakula unga wetu ()

Mariam na Pendo anaondoka keshokutwa ()

Asante kwa ushirikiano wako